CHUO CHA BIBLIA

I& II WAFALME, I& II MAMBO YA NYAKATI, EZRA / NEHEMIA NA ESTA

KITABU CHA NNE

VITABU VYA 1 & 2 WAFALME

SURA YA KWANZA

Wafalme Na Manabii

Baada ya kuachana na vitabu vya Samweli, sasa tunaingia katika sehemu ya vitabu vya Wafalme wa Kwanza na Wa pili. Huku tukisoma hivi vitabu, tilia mkazo dhana kuu mbili: (1) Jinsi Mungu alivyowapa fursa kuu wana wa Israeli huku wakiwa wamenaswa katika upinde wa kuasi na kurudi nyuma, na (2) Uvumilivu wake Mungu kwa kuhusika na baadhi ya wafalme waovu. Dhana hizi zitakuwa kama misingi dhabiti tunaposhuka chini kutoka vilele hadi bonde zakustaajabisha kwenye vitabu vya historia ya Waebrania.

Ukaguzi Wa Wafalme Pamoja Na Milki

Vitabu vya wafalme wa Kwanza na wa Pili vinatueleza juu ya ufalme wake mwanadamu ambao ulitokana na Israeli kumkataa Mungu kuwa ni mfalme wao. Katika Wafalme wa Kwanza, tunajifunza kuhusu mgawanyiko wa ufalme wa kibinadamu. Nao katika Wafalme wa Pili, tunakumbana na utekaji nyara wao wenye kuhuzunisha.

Tutakumbana na onyo nyingi katika vitabu vya Ufalme, kwa kuwa wengi wa wafalme walikuwa waovu. Matokeo yake kwa watu yalikuwa mabaya mno, yamkini unaweza kukumbuka kwamba Mungu hakuwajibika kwa matokeo yao yote. Watu waliwajibika kwa kuwa wao ndio walitaka wale wafalme-nao wafalme waliwajibika kwa maovu yao wenyewe.

Umuhimu wa vitabu hivi viwili ni kwamba, vinazungumzia juu ya mgawanyiko, kuanguka, pamoja na kutekwa nyara kwa Israeli na Yuda. Tunaweza kuvitaja vitabu vya Wafalme wa Kwanza na wa Pili kama, ‘Kunawiri na Kuporomoka kwa taifa la Waebrania.’ Wafalme wa Pili sura ya kumi na saba inaeleza utekaji nyara wa Ashuru kwa taifa la kaskazini, yaani makabila kumi yaliyojumuisha taifa la Israeli. Wao walifanya msafara huku wakiwa wamefungwa kwa minyororo hadi Ashuru, na kufuatia tukio hilo, hawajawahi kusikika tena katika maandiko. Wakati mwingi wao hutajwa kama, ‘makabila yaliopotea ya Israeli.’

Katika 2 Wafalme sura ya Ishirini na tano, tunasoma kuhusu tukio mbovu kuhusu kufungwa kwa taifa la kusini yaani Yuda na mfalme Nebukadreza pamoja na Wakaldayo. Mateka ambao hawakuuawa walichukuliwa hadi Babeli wakati Yerusalemu ilipoanguka. Miaka sabini baadaye, Waajemi *(Persians*) waliuteka mji wa Babeli. Koreshi Mkuu, mfalme wa Uajemi, aliongozwa na Mungu kutangaza kuwa ye yote wa asili ya Kiyahudi aliyeishi Uajemi yuko huru kurudi Israeli na kulijenga hekalu, mji, na nchi yao.

Kihistoria, kilichofuata kilikuwa ni 'vitabu vya baada ya Kutekwa kwao.' Ezra, Nehemia, pamoja na Esta vinatufahamisha juu ya kurudi kwa baadhi ya wana wa Israeli kutoka utumwani huko Babeli. Kitabu cha Esta kitaeleza baadhi ya mambo yaliotukia huko Mede na Uajemi, miongoni mwa wana wa Israeli waliochagua kutorudi Yerusalemu. Tutakapomaliza kukikachambua kitabu cha Esta, tutakuwa tumemaliza somo letu katika vitabu vya historia vya Agano la Kale.

Kutana Na Manabii

Manabii wote ambao waliandika vitabu vya unabii katika Agano la Kale watoshea mahali fulani katika sehemu ya historia iliyomo katika vitabu vya historia. Tutakutana na manabii hawa kwa karibu na kwa kibinafsi baada ya kumaliza ukachuguzi wetu wa vitabu vya Mashairi vilivyo katika Agano la Kale.

Kwa Hivyo, Nabii Ni Akina Nani?

Hebu tutilie maanani yale ambayo nabii alikuwa. Neno hili nabii linamaanisha 'kuzungumza kwa niaba ya Mungu.' Ni neno ya Kiyunani (Kigriki), yaani maneno mawili yaliyounganishwa na kuwa neno moja: (Pro,) ambalo linamaanisha, 'Kusimama mbele ya', pamoja na (Phano), ambalo linamaanisha 'kutia mwangaza.' Haya ndiyo hawa manabii waliyoyatenda. Manabii walihubiri neno lake Mungu lililoandikwa (Vitabu vyake Musa). Pamoja na hayo, waliupokea ufunuo kutoka kwake Mungu. Kuongezea hayo, wao 'walinena wazi', wao walilinena neno lake Mungu na kulitangaza wazi. Hii inamaanisha kwamba wao walikuwa wahubiri. Lakini wakati mwingine, waliyanena yatakayotukia hapo baadaye. Kutabiri huku kunatuvutia sisi mno, lakini kazi yake huyu nabii ilikuwa kulihubiri neno lake Mungu. Nabii alisimama katikati ya Neno lake Mungu na watu wake na kulifanya Neno hilo kutangazwa kwa watu hao. Huduma yao ilikuwa wakati mwingi ni kukumbana ana kwa ana, kwa hawa watu waliokuwa wakiasi kinyume chake Bwana; naye Mungu alihitaji kuwakemea kupitia nabii wake waliokuwa waaminifu.

Katika Wafalme wa Kwanza, nabii mkuu ni Eliya, ilhali katika Wafalme wa Pili ni Elisha ambaye ni mrithi wake Eliya. Ingawaje tutatilia mkazo hawa manabii wawili tunapovichunguza vitabu vya Wafalme, ningependa kuhakikisha kwamba hatutaepuka kuwafahamu baadhi yao ambao hawafahamiki mno. Katika Wafalme wa Kwanza sura ile ya Ishirini na mbili, utakutana na mmoja wao ambaye anajulikana kama Mikaya.

Wakati ufalme ule ulipogawanyika, wafalme hao walikuwa wakikutana pamoja mara kwa mara ingawa kwa wakati mwingi wao walikuwa maadui. Kumbuka hivi, wafalme wote waliokuwepo Kaskazini walikuwa waovu na waasi. Ufalme wa Kusini wa Yuda ulikuwa na mfalme mwema mara kwa mara. Hakuna aliyekuwa mwema kama Daudi, hata hivyo, baadhi ya wafalme walikuwa wamcha Mungu, kama Hezekia, Yehoshafati na Yosia.

Katika Wafalme wa Kwanza sura ya ishirini na mbili, mfalme wa Israeli, Ahabu, pamoja na mfalme wa Yuda Yehoshafati, walikutana pamoja katika kongamano kuu. Ahabu alikuwa mtu mwovu mno, ilhali huyu Yehoshafati alikuwa wa kadiri ya wastani. Je, walikuwa wakifanya jambo lipi pamoja? Wao walikuwa na wajukuu kwa kuwa wana wao walikuwa wameoana. Lakini sababu kuu ya kongamano yao ilikuwa kwamba huyu Ahabu alikuwa akitaka kufanya vita. Kwa hivyo, alimtaka huyu Yehoshafati kumsadia dhidi ya Shamu.

Yehoshafati aliitikia mwito wake Ahabu baada ya kuhakikishiwa na manabii. Kihistoria, wakati huo ilikuwa ni desturi yao kuhakikishiwa na manabii juu ya jambo lo lote lile walilotaka kutenda. Ahabu alisema, *'Wewe unahitaji manabii? Nitakupa manabii. Mimi ninao mia nane hamsini – manabii wake Baali pamoja na miungu iliyotambulikana sana.'* Hao manabii wa uongo walimhimiza Ahabu kwenda vitani na kumwahidi ushidi. Lakini Yehoshafati alitaka kusikia kutoka kwake nabii wa kweli wake Mungu aliye wa kweli, Yahwe.

Kwa kusitasita, huyu Ahabu akasema, *'Yupo mtu mmoja, ambaye tungeweza kumwuliza Bwana kwa sababu kwa yeye, yaani Mikaya mwana wake Imla; lakini namchukia; kwa sababu hanibashirii mema, ila mabaya.'*(8). Yehoshafati akasema, *'Nenda ukamlete yeye.'* Hivyo basi, Ahabu akamtuma akida kwake Mikaya.

Huku wakisafiri kwa farasi, akida huyu alimsihi Mikaya kuutoa unabii unaoambatana na wale manabii wengine. Lakini Mikaya akasema, *'Kama Bwana aishivyo, neno lile Bwana aniambialo, ndilo nitakalolinena.'* (14).

Mikaya alipoletwa mbele za hawa wafalme wawili katika kasri la kifalme, kulikuwepo na sherehe, Ahabu akasema*, 'Je! Mikaya? Tuende Ramoth-Gileadi kupiga vita, au tunyamaze?'* Naye Mikaya akasema, *'Kwea, ufanikiwe; kwa kuwa Bwana atautia mkononi mwa mfalme.'* Ahabu alipigwa na butwaa na kusema, *' mara ngapi nikuapishe usiniambie neno ila yaliyo kweli, kwa jina la Bwana?*' Naye Mikaya akamjibu*, 'Naliwaona Waisraeli wote wametawanyika milimani, kama kondoo wasio na mchungaji.'* Ahabu akasema*, 'Je! Sikukuambia hatanibashiria mema, ila mabaya?'* (15-18).

Hata hivyo, Ahabu na Yehoshafati, waliamua kwenda vitani kinyume na kupigana na taifa la Shamu bila kujali lo lote. Lakini Mikaya akawaambia bayana kwamba wao walikuwa wakiufuata uongo: *'Nilimwona Bwana ameketi katika kiti chake cha enzi, na jeshi lote la mbinguni wamesimama upande wa mkono wake wa kuume na wa kushoto. Bwana akasema, Ni nani atakayemdanganya Ahabu, ili akwee Ramoth-Gileadi akaanguke?…..Akatoka pepo, akasimama mbele za Bwana, akasema, Mimi nitamdanganya. Bwana akamwambia, Jinsi gani? Akasema, Nitaondoka, na kuwa pepo wa uongo kinywani mwa manabii wake wote. Akasema, Utamdanganya, na kudiriki pia; ondoka ukafanye hivyo.* (19-22).

Ahabu akamwamuru Mikaya kutiwa gerezani na kulishwa kwa chakula cha shida, na maji ya shida, hata atakaporudi kwa amani. Mikaya akasema, *'Ukirudi kabisa kwa amani, Bwana hakusema kwa mimi.'*(28). Ahabu na Yehoshafati waliwaongoza majeshi yao kinyume dhidi ya Shamu. Nasi tunaweza kudhania kwamba Mikaya alikufa huku akila mkate na kunywa maji kwenye jela, kwa kuwa huyu Ahabu hakurudi tena.

Katikati mwa vita vikali, unabii wake Mikaya ulitimizwa kikamilifu. Majeshi yake Ahabu na Yehoshafati yalitawanyika kote milimani kama kondoo walio na mchungaji. Mwanajeshi wa Shamu alivuta upinde wake kwa kubahatisha, akampiga Ahabu mahali ambapo pa kuungana mavazi yake ya chuma. Ahabu alijehuriwa sana na akafa huku majeshi yakirudi nyumbani yakiwa yameshindwa.

Wapo wengi ambao hawajatajwa majina, manabii wasiofahamika katika vitabu vya Wafalme. Kwa mfano, Wafalme wa Kwanza sura ya kumi na tatu, nabii ambaye hajatajwa jina alimkabili

mfalme mwovu Yeroboamu. Yeroboamu alinyosha mkono wake kwa nabii na kusema, *'Mkamateni*.' Bali ule mkono wake aliounyossha ukakatika, wala hakuweza kuurudisha kwake tena. Halafu mfalme akamsihi yule nabii kwa kusema, 'Umsihi sasa Bwana, Mungu wako, ukaniombee, ili nirudishiwe mkono wangu tena!' Hivyo basi, nabii huyo akayakubali maombi yake Yeroboamu, na kumwomba Bwana mkono wa mfalme ukarudishwa tena, ukawa kama ulivyokuwa kwanza.

Unapoendelea kusoma kuhusu hawa manabii, utafahamu kwamba wote walikuwa na nguvu zake Mungu zilizotenda kazi kupitia wao. Na bila miujiza yake Mungu, hawa manabii hawangeweza kuwakabili wafalme waliokuwa waovu.

Jinsi ambavyo tayari tumetambua, Eliya, ndiye nabii mkuu ambaye tunakumbana naye katika kitabu cha Wafalme wa Kwanza. Katika Wafalme wa Kwanza sura ile ya kumi na nane, Eliya alipata fursa ya kunawiri. Watu wake Mungu katika falme zote mbili walikuwa kwa muda mrefu kana kwamba wameasi Mungu na kuigeukia miungu ya uongo. Walikuwepo manabii wengi waliokuwa wakiwakilisha miungu ya uongo. Eliya aliwatia changa moto manabii mia nane na hamsini wake malkia Yezebeli, mkewe Ahabu katika mashindano. Kila upande utajenga madhabahu, na kuweka juu yake dhabihu, kisha kuomba Mungu kutuma moto na kuiteketeza dhabihu ile. Ikiwa Mungu atawajibu kwa moto wa kimiujiza na kuteketeza ile dhabihu, basi hiyo ingekuwa dhihirisho ya wazi kwamba yatokana nao manabii wa kweli wake Mungu wa kweli.

Kulingana na umati uliokusanyika katika Mlima Karmeli, manabii wa uongo wake Baali walizidi kuomba kwa nguvu pamoja na kujikata kwa visu na vyembe kama ilivyo desturi yao, hata damu ikawachuruzika na kujipiga mijeledi ili kwamba wapate kusikika naye Baali. Ikiwa wakati wa adhuhuri ulipofika, Eliya alianza kuwafanyia dhihaka kwa kusema: *'Mwiteni kwa sauti kuu; maana ni mungu huyo; labda anazungumza, au ana shughuli, au anasafiri, au labda amelala, sharti aamshwe!'* (27). Wao walizidi kupiga kelele, kwa majonzi mengi hadi ilipofika jioni. Mwishowe, wakakata tamaa.

Eliya alifanya mfereji, kama wa vipimo viwili vya mbegu, ukiizunguka madhabahu. Kisha akaomba maombi makuu na ya imani: *'Ee Bwana, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako. Unisikie, Ee Bwana, unisikie, ili watu hawa wajue ya kuwa wewe umewageuza moyo wakurudie.'* (1 Wafalme 18:36-37).

Ndipo moto wa Bwana ukashuka, ukaiteketeza sadaka ya kuteketezwa, na kuni na mawe, na mavumbi, ukayaramba yale maji yaliyokuwamo katika mrefeji. Na watu wote walipoona, wakaanguka kufudifudi; wakasema, *Bwana ndiye Mungu! Bwana ndiye Mungu!'* (39). Huu kwa hakika ulikuwa ni uamsho mkuu mno! Baadaye watu wake Mungu waliwaangamiza manabii wote mia nane na hamsini wa uongo. Siku ile juu ya Mlima Karmeli ilikuwa ndio wasaa wake Eliya wa Kunawiri.

Katika sura ifuatayo, labda unaweza kukosa kumtambua huyu Eliya. Mke wake Ahabu, yule Yezebeli, ambaye aliazisha kuabudu Baali huko Israeli, alikasirishwa sana na kuangamizwa kwa manabii wake. Hivyo basi, akamtisha kumwangamiza Eliya. (19:2). Naye Eliya aliyekuwa shujaa asiye na woga na akatoroka huko nyikani, na akaketi chini ya mteremu huku amechoka na kujiombea roho yake afe. Yeye alikuwa amevunjika moyo kabisa.

Shida moja ya Eliya ilikuwa ni uchovu mwilini mwake. Kwa hakika, hoja bora katika Wafalme wa Kwanza sura ile ya kumi na tisa ni: 'Jinsi ya kufanyika mchovu, kimwili, kihisia, na kiroho.' *'Akafika kunako pango, akalala ndani yake. Na tazama, neno la Bwana limkamjia, naye akamwambia Unafanya nini hapa, Eliya?'* (9).

Je, Mungu amewahi kukuliza swali hilo? Sijui wewe upo mahali gani kiroho. Labda Mungu anataka kukuuliza wewe kuipitia hadithi yake Eliya, 'Unafanya nini hapa?' Je, wewe upo mahali pale Mungu anataka wewe kuwa?

Hebu nikukumbushe kwa mara nyingine kwamba wahitajika kuitafuta mifano na maonyo katika vitabu vya Wafalme. Katika vitabu hivi, utakumbana na maonyo ya kushangaza mno na hasa katika maisha yao wafalme waovu. Na pia utakutana na mifano mikuu katika maisha ya manabii, hasa manabii kama Eliya, Elisha, na Mikaya.

SURA YA NANE

Kunawiri Pamoja na Kuanguka kwa Ufalme

Tunaposoma Wafalme wa Kwanza na wa Pili, tunajifunza kuhusu kunawiri pamoja na kuanguka kwa ufalme ambao wana wa Israeli walikuwa wakitaka. Kilele cha ufalme huo wa

Kiyahudi kulifika wakati Sulemani alipokuwa akitawala. Lakini haukudumu kwa muda mrefu, kwa kuwa ilikuwa ni tukio la hiari ya mapenzi yake Mungu (*permissive will),* na wala si mwongozo dhahiri wake*. (Directive will).*

Katika Wafalme wa Kwanza, tunasoma maelezo kuhusu jinsi ufalme ulivyogawanyika. Ilhali katika Wafalme wa Pili, tunasoma jinsi ufalme wa kaskazini na wa kusini ulivyosambaratika. Ufalme wa kaskazini wa Israeli, ulifutiliwa mbali na Ashuru; ilhali ufalme wa kusini, yaani Yuda, ulitekwa na kuhamishwa hadi Babeli.

Ukitazama kwa makini kuhusu kusambaratika kwa ufalme wa kusini, utagundua kwamba kuwekwa chini ya kongwa la utumwa na katika uhamisho hakukuwa rahisi. Kwa hakika, Yerusalemu ilianguka mara tatu katika muda wa miaka ishirini. Mara ya kwanza, Yehoyakimu aliusalimisha mji ule na kumtumikia mfalme wa Babeli kwa muda wa miaka mitatu. Baadaye, aliasi kinyume cha majeshi yaliokuwa yakiusimamia utawala wa Babeli, na iliwabidi kunyakua ule mji kwa mara nyingine ya pili. Kuanguka kwa pili kwa mji wa Yerusalemu kulitukia wakati ambapo mwanawe Yehoyakimu, Yokonia alipousalimisha mji ule, nao wana wengi wa Israeli wakapata kuangamizwa. Wale walionusurika maafa walichukuliwa mateka hadi Babeli. Nao Wababeli wakamfanya Sedekia kama mfalme kibaraka au kaimu mfalme huko Yerusalemu. Taratibu hiyo ilidumu kwa muda wa miaka kumi. Lakini Sedekia pia aliasi, na hivyo mji ule ukatekwa kwa mara nyingine ya tatu. Hii ndiyo iliyokuwa mara ya mwisho ya kuanguka kwa mji wa Yerusalemu chini ya uharibifu na utekaji nyara – mji wote uliharibiwa na kuteketezwa moto hadi kuwa majivu.

Hebu tusitembee kabla ya kutambaa. Hebu turejee nyuma hadi nyakati za kunawiri kwa ufalme huo, wenye kunawiri na kusifika na wenye utajiri mkuu chini ya utawala wa Sulemani. Yeye ni kielelezo kwetu cha kuigwa na pia ni onyo kwetu la kuepukwa.

Urithi Wa Utawala Wenye Kuvurugikana Wake Sulemani

Sulemani anafanana sana na Sauli ambaye alikuwa na mwanzo mwema lakini alimalizia vibaya. Mwanzoni ambapo Daudi alipomkabidhi huyu Sulemani mamlaka ya kuwa mfalme wa tatu wa Israeli, ilionekana kwamba yeye angefuata mfano wa babake Daudi na kuzifuata nyayo zake. Na kwa kunyenyekea kwingi, alimwomba Mungu ampe hekima ili awaongoze watu Wake. (1 Wafalme 3). Neno hilo lilikuwa jema machoni pa Bwana, ya kuwa Sulemani ameomba neno hilo. Baadaye alimpa moyo wa hekima na wa akili, mali na fahari.

Sulemani alifanyika kuwa mtu tajiri na mwenye hekima kuliko ye yote aliyepata kuishi. Yeye ni mfano bora wakati ambako anamwomba Mungu ampe hekima na wakati ambapo aliweka ombi hili mbele kabla ya utajiri au haja za kibinafsi. Lakini bali na haya yote, alikuwa ndiye wa mwisho kabisa na mwenye kusambaratika zaidi ya ye yote aliyewahi kuishi. Kumbuka: Mgawanyiko, Kusabaratikana, Na Utekaji chini ya kongwa la utumwa kwa ufalme hazikuwa kwa sababu ya dhambi yake Daudi. Daudi alikuwa ametubu dhambi yake, naye Mungu akamsamehe. Maovu yote ambayo yaliupata ufalme huu yalikuwa kwa sababu ya dhambi yake Sulemani na matokeo ya kushindwa kwake.

Wakati ufalme wa Israeli ulipofikia kilele chake cha kunawiri, Sulemani aliasi Mungu na kuwageukia miungu wengine. Wake zake Sulemani mia saba na suria mia tatu walikuwa waabudu wa miungu mingine, na kwa bahati mbaya akawafuata katika jambo hilo la kuabudu sanamu.

Naamini kuwa baadaye, huyu Sulemani alipata kumrudia Mungu wa kweli. Katika kitabu cha Zaburi mia moja ishirini na saba, Zaburi ambayo huyu Sulemani aliandika, alisema haya, *'Bwana asipoijenga nyumba yeye waijengao wafanya kazi bure.'* (1). Sulemani alikuwa mjenzi hodari, na siyo tu katika ujenzi wa Hekalu, bali pamoja na miji, bustani na merikebu. Katika Zaburi hii yake, yeye atupatia mafunzo kuhusu utaratibu wa kutenda mambo. Ujumbe wake Sulemani ni huu: 'Inawezekana kabisa kutilia mkazo mambo yasiyo muhimu, na kufanya kazi kwa ubatili tu, pia inawezekana kufanya ujenzi bure kwa kuwa inawezekana kuwa na mwelekeo, kufanya kazi na kujenga mambo yaliyo mabaya. Ujuzi sio mwalimu wa pekee, ingawa ni mwalimu mwenye ushawishi mwingi. Ipokee faida kutoka kwa ujuzi wangu. Jambo ambalo muhimu zaidi ambalo utawahi kulijenga katika maisha yako ni maisha ya mwanao.'

Wanawe Sulemani walikuwa waovu. Mwanawe ambaye aliurithi uongozi wake alikuwa mpumbavu. Ni wazi kabisa kwamba Sulemani alijuta sana kwa kutumia wakati mwingi katika ujenzi wa mambo yote yaliyomo chini ya jua isipokuwa maisha ya wanawe. Zaburi 127 yaonyesha kwamba lengo zake Sulemani zilikuwa bila sababu muhimu maishani mwake akiwa mtu mzima.

Katika kitabu cha Mhubiri, Sulemani anatufafanulia zaidi kuhusu ujumbe huu wake katika Zaburi tuliyoitaja hapo jawali. Kitabu cha Mhubiri kilikuwa ni mahubiri ambayo Sulemani alitoa kwa vijana wachanga ambao walikuwa raia wake katika milki ambayo alikuwa kiongozi mfalme. Mahubiri

hayo pamoja na Zaburi hii yanatupatia sababu ya pili kuamini kwamba yeye alikuwa na ujuzi wa kiroho wa kumrudia Mungu mwishoni mwa maisha yake duniani.

Sababu ya tatu ya kuamini kwamba Sulemani alirudi kwake Mungu ni wakati ule wa kihistoria ambao umenakiliwa tena katika Mambo ya Nyakati wa Pili, siyo tu kwamba dhambi yake Daudi ilifutiliwa mbali bali, pia hata ile yake Sulemani. Hii inamaanisha Sulemani, kama baba yake, lazima alitubu pamoja na kuiungama dhambi yake.

Sulemani kwa hakika anaonekana kwa udhahiri mwingi katika maandiko yaliyo katika vitabu vya kihistoria kama mmoja wa onyo kuu. Unapokisoma kitabu cha Wafalme wa Kwanza, Sulemani ndiye mfalme muhimu zaidi ambaye unahitaji kutilia maanani maonyo pamoja na mifano yake.

Mfalme Mwema, Lakini Mwenye Udhaifu – Mfalme Hezekia

Hezekia alikuwa ni mmoja wa wafalme wa Yuda wakuu waliochelea (tazama 2 Wafalme 18-20). Aliitakasa nchi yake kutokana na ibada ya sanamu iliyokuwa imekolea kote na kuota mizizi, naye akamtumainia na kumtii Mungu. Kwa hakika, hakuna mfalme ye yote kabla yake au baada yake aliyekuwa karibu naye Mungu kama yeye. Hivyo basi, yeye ni mfano bora kwetu, lakini pia anatupa maonyo fulani.

Wakati Hezekia alipokuwa katika hatari ya kufa kwa ugonjwa, Mungu alizungumza naye kupitia nabii Isaya, na kumwambia kwamba atengeneze mambo ya nyumba yake maana angekufa. (20:1-11). Baada ya kusikia hivyo, Hezekia alijigeuza na kuelekeza uso wake ukutani, na kumlilia Mungu ili apate kuhifadhi uhai wake. Baadaye, tunasoma ujumbe huu wa kuvutia ambao Mungu alimpelekea Hezekia kwa kupitia nabii Isaya: *'Nimeyasikia maombi yako, na kuyaona machozi yako.'* (5). Mungu huyaona machozi. Nadhani hili ni jambo muhimu. Naye Mungu akamzindishia miaka ya ziada kumi na mitano katika maisha yake Hezekia. Huu ni mfano bora kwetu. Mtu huyu bado alikata rufani kwake Mungu, ingawaje alikuwa ameambiwa kwamba angefariki na nabii mkuu Isaya; ambaye alikuwa akizungumza kwa niaba ya Bwana Mungu.

Hata hivyo, Hezekia alifanyika kuwa onyo katika tukio ambalo lilikuwa na uhusiano na muijiza huu. Siku moja Wababeli walimtembelea Hezekia, naye akawaonyesha nyumba yote yenye kila kitu – zana zake za vita, silaha, pamoja na mali yake yote. Baadaye, Isaya akamwuliza, *'Wameona nini nyumbani mwako?'* (15). *'Vitu vyote vilivyomo nyumbani mwangu wameviona,'* Hezekia akamjibu.

Isaya akamwambia kwamba hili lilikuwa kosa kubwa mno, kwa sababuhiyo, *'Angalia siku zinakuja, ambazo vitu vyote vilivyomo nyumbani mwako, na hivyo vilivyowekwa akiba na baba zako hata leo, vitachukuliwa mpaka Babeli; hakitasalia kitu, asema Bwana.'* (17). Isaya alikuwa akitabiri kuhusu uvamizi na utekaji wa Wababeli dhidi ya mji wa Yerusalemu. Kulingana na unabii wake Isaya, wanawe Hezekia wangelifanywa kuwa matowashi na kupelekwa kama mateka huko Babeli. (18).

Je, mfalme alikabiliana vipi na ujumbe huo? Yeye aliridhika kwa kuwa mambo haya yote hayangelimtokea. *'Je! Sivyo, ikiwapo amani na kweli katika siku <u>zangu?</u> Yeye akasema.'* (19). Yeye kwa kutokujali akalikubali neno lake Mungu kwa kuwa yeye aliamini kwamba miaka kumi na mitano aliyoongezwa ilikuwa bora. Yeye hakuonekana kujali yale ambayo yangewakuba wanawe pamoja wa wajukuu wake. Huku kujipenda kibinafsi kwake huyu Hezekia hakukumfanya kuwa mfano bora wake baba mzazi au tabia njema ambayo inaweza kuigwa kwa baba mzazi bora. Kwa sababu ya nia hii yake, maisha yake ni onyo kwetu tulio baba wazazi.

Elisha, Mfano Bora

Tuna mfano mwingine ulio bora katika maisha yake nabii Elisha. Katika Wafalme wa Pili sura ya tano, jemadari mkuu katika jeshi la Shamu alikwenda kwake nabii huyu ili kupokea uponyaji. Kwa wakati huu, Shamu ilikuwa ikijitayarisha kuvamia ufalme wa kaskazini wa Israeli. Tayari vita vidogo vilikuwa vimezuka kwenye mipaka yao. Wao walikuwa na jeshi hodari, lakini jemadari mkuu wao, Naamani alikuwa akiugua na ugonjwa wa ukoma. Mfungwa kijana mwanamke kutoka nchi ya Israeli, aliyemhudumia mkewe Naamani, aliwapasha habari kuhusu nabii aliyeko Samaria katika nchi ya Israeli aliyekuwa na nguvu ya kuponya ugonjwa wa ukoma. Hivyo basi, huyu Naamani akalichukua farasi na magari yake pamoja na baadhi ya askari katika jeshi lake kuelekea kwa nabii Elisha.

Naye Naamani alikuwa na dhana mbovu kuhusu jinsi ambavyo Elisha angelimponya. Huyu Jemadari mwenye uwezo mwingi alidhani kwamba kungalikwa na ramsha ramsha nyingi. Lakini Elisha hakutoka nje ya chumba chake na kumwamkua huyu Jemadari. Badala yake, alimtuma mtumishi wake aitwaye Gehazi kwake huyu Naamani, ambaye alimwambia, '*Tazama Bwana wangu asema, Enenda ukaoge katika Yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia, nawe utakuwa safi.'* (10). Naamani alipandwa na hasira! Akalipindua gari lake na kuondoka kwake Elisha kwa kisulisuli kingi, huku akiwaambia watumishi wake, *'Tazama, nalidhania, Bila shaka atatoka kwangu, na kusimama, na kuomba kwa jina la Bwana, Mungu wake, na kupitisha mkono wake mahali penye ugonjwa, na kuniponya mimi mwenye* ukoma.' (12). Alifikiri kuwa katika nchi yake,

kulikuwa na mito mingi iliyokuwa bora, naye hakuwa tayari kwenda na kujitosa ndani ya mto wenye tope jingi kama Yordani.

Hata hivyo, watumishi wake Naamani walimhimiza kufuata maagizo yake Elisha, naye baadaye akabadilisha mawazo yake na kujitosa mwenyewe ndani ya Yordani mara saba. Naye alipopanda juu kutoka majini kwa mara ya saba, ukoma wake ulikuwa umetoweka! Haikutokea kama yeye alivyokuwa akitarajia, lakini matokeo yalikuwa bora kuliko alivyokisia.

Hadithi hii ya uponyaji wa Naamani ni fumbo la funzo la kuvutia kuhusu wokovu. Wengi wa watu wenye njaa kuu ya kiroho ambao humjia Kristo kwa wokovu huwa na dhana nyingi kuhusu jinsi wokovu wao utakavyokuwa. Wengine hudhania kwamba wokovu utakuwa jibu kwa kila kitu, katika elimu ya kithiolojia. Wengine hufikiri kwamba wokovu ikiwa hauna ugumu wo wote basi si wokovu. Huu ni ukweli mkuu hasa kwa watu ambao wamo katika ulimwengu na jamii ya elimu. Wao wanaposikia kuhusu jinsi injili ilivyo rahisi, huwa wanaiona kana kwamba ni nyepesi sana hivi kwamba hawawezi kuliamini. Lakini kwa hakika, injili ni nyepesi, jinsi ilivyo kujitosa ndani Yordani mara saba, na hakuna anayehitaji usanifu au elimu ye yote ili kupokea wokovu huo. Elisha ni mfano bora kwa kuwa yeye hakuyakaribisha matarajio yake Naamani, ingawaje angefaidika sana kwa kufanya hivyo. Hili ndilo somo kuu katika historia yake huyu Naamani mwenye ukoma pamoja na nabii Elisha.

Kabla ya kumaliza kusoma vitabu hivi ambavyo vinafafanua ufalme wake Mungu, hebu tuwatazame manabii kwa mara nyingine na tumchambue wa mwisho wao. Manabii hawakuwa tu watu walionena kwa niaba yake Mungu, au watu Mungu alionena kuwapitia; wao hawakuwa tu watu waliosimama mbele ya Neno lake Mungu na kulipatia mwangaza; bali wao walikuwa watu waliokuwa wameinuliwa naye Mungu wakati kulipokuwepo na shida. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kwamba, ‘Hakuna shida, hakuna Nabii.’ Lakini punde tu wakati shida inapozuka, unaweza kumtarajia nabii.

Kwa mfano, wakati wote kazi ya Mungu inapokumbana na pingamizi lo lote lile, Mungu alimwinua Nabii. Kazi moja ya nabii wa Mungu ilikuwa kufanya mahubiri yake kugusia pingamizi lililopo hadi litakapoondoka na kazi yake Mungu iendelee mbele. Kuondoa shida na pingamizi ambazo zilizuia kazi yake Mungu ilikuwa ndio wajibu mkuu wake nabii.

Kwa ufupi, ikiwa unaweza kusoma Wafalme wa Kwanza na wa Pili, hebu tambua kunawiri na kuanguka kwa Ufalme. Unapozidi kujifunza kuhusu ufalme huu, utaweza kupambanua yale ambayo Mungu ataka kuyatenda siku ya leo kupitia Kanisa lake. Halafu, watazame wafalme kwa makini sana. Jinsi ilivyo maisha yao ni onyo kwetu sisi; baadhi yao wachache ndio mfano bora kwetu. Kisha wafuate manabii kwa uangalifu, kwa kuwa kwa wakati mwingi, wao ni mifano bora tuwezayo kuiga.

Maandiko yaliyomo katika Wafalme wa Kwanza na wa Pili yanajumulisha sehemu kubwa ya kusomwa; lakini katika somo kama hili letu, sisi tutachunguza huku tukijaribu kuviweka hivi vitabu katika mtazamo bora ili kwamba katika wakati ambapo wewe utakapokuwa ukivisoma, utajifunza mengi zaidi kutoka kwavyo. Hivyo basi, haya ni machache kuwahusu Wafalme.

Baadhi ya Maoni ya Mwisho kuhusu 1 Wafalme na 2 Wafalme.

Jambo la kwanza, tunafaa kutambua jinsi Mungu alivyowavumilia kwa muda wafalme ambao kwa hakika yeye hakuwataka kuitawala Israeli. Hebu tambua uvumilivu wake kwa wafalme waovu, na hasa katika ufalme wa Kaskazini. Unaweza kutambua jinsi alivyowambembeleza kwa uvumilivu mwingi hawa wafalme na kuwaonya kabla ya misiba na mikasa ya uvamizi kuwaangukia. Mwishowe, waweza kutambua kwamba Mungu pia aliyajibu maombi ya wafalme waovu, na jambo hili linazusha maswala ya ubishi kithiolojia (2 Wafalme 13:4-5). Watu wengi huamini kwamba Mungu huyasikia maombi ya wale wanaoamini tu, walio katika ushirika pamoja naye. Jambo hili halipatikani katika maandiko. Mungu aliyasikia maombi yake mtoza ushuru. (Luka 18:10-14). Yesu aliyasikia maombi yake mwizi aliyesulubiwa juu ya msalaba (Luka 23:42,43), naye Mungu pia aliyasikiliza maombi ya hawa wafalme waovu. Siku ya leo kama mwanawe mtu muovu akijeruhiwa kwenye ajali, ikiwa mtu yule atamwomba Mungu apate kuyanusuru maisha ya mwanawe, je Mungu anaweza kujibu maombi yale? Naamini kwamba Mungu anaweza kuyasikia maombi yake kila mtu, wakati wo wote! Ukweli huo unaonyeshwa kwetu katika kitabu cha Wafalme.

SURA YA TISA.

Mambo Ya Nyakati ‘Mambo Yaliyoachwa.’

Utangulizi Wa Mambo Ya Nyakati 1 Na 2.

Historia ya vitabu vya Samweli na Wafalme ni sawa na ile ya vitabu vifuatavyo, Mambo ya Nyakati 1 na 2 katikati ya miaka 1000 kabla ya Kristo hadi 500 pia kabla ya kuzaliwa kwake Kristo. Mpangilio wa vitabu vilivyotangulia unaviweka vitabu vya Mambo ya Nyakati, Ezra na Nehemia kwa wakati mmoja. Kiebrania kinachotumika katika Mambo ya Nyakati kinafanana na kile kilio katika vitabu hivyo, hivi kwamba wasomi wengi huamini kwamba ni Ezra aliyeviandika vitabu hivi vitatu. Ni baadaye ambapo vitabu hivi vinawekwa katika kundi moja na Samweli na Wafalme kwa sababu ya kulingana na nyakati zake.

Sababu Ya Marudio.

Ni kwa sababu gani Mungu ananakili kwa mara ya pili nyakati hizo za kihistoria? Kuna baadhi ya majibu. Kwanza, marudio ndiyo kina kikuu cha elimu. ‘ikwa haufanyi marudio, basi wewe haufundishi.’ Ndivyo wasemavyo wakufunzi. La pili, katika maandiko, marudio siyo ya kufunza tu, bali ni ya kutilia mkazo. Hebu tilia maanani yale ambayo yanarudiwa katika maandiko. Habari kuhusu uumbaji zinaelezewa mara mbili katika kitabu cha Mwanzo. Sheria yake Musa iliyo katika kitabu cha Kutoka inarudiwa mara nne katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati. Historia ya maisha yake Yesu Kristo inarudiwa mara nne katika Agano Jipya. Na wakati huu wa historia yao Wayahudi historia iliyo kwenye nakili ya maandiko ya kihistoria inarudiwa tena katika Mambo ya Nyakati.

Ni jambo lipi ambalo linatiliwa mkazo katika kitabu cha Mambo ya Nyakati? Ni wazi kwamba, jibu kwa swali hilo ni: Ufalme wake Mungu. Yesu alisema kwamba ufalme wake Mungu watahitajika kuichukua nafasi ya kwanza katika maisha yetu na sehemu kuu katiika maombi yetu; kwa hivyo, hiki ndicho kina kikuu cha kuzaliwa upya. (Mathayo 6:33; Yohana 3:3,5). Hivyo basi, katika utangulizi wetu wa dhana hii kuhusu ufalme wake Mungu ambayo tunaisoma katika maandiko ya kihistoria ni muhimu sana. Mungu anataka tufahamu dhana kwamba Yeye ni Mfalme, na anataka tufanyike raia watiifu katika ufalme wake siku ya leo. Hii ndiyo sababu Mungu anarudia nyakati za historia hii.

Sababu nyingine ya tatu ya kufanya marudio kwa mfumo huu ni kuwa, Mungu anataka sisi kufahamu kwamba watu wake walimkataa Yeye kuwa mfalme wao na hivyo sisi tunaishi pamoja na matokeo ya kumkataa huko. Mungu pia anataka sisi kufahamu kumkataa huko, kwa kuwa hii ni picha ambayo inatuonyesha maisha jinsi yalivyo na vile tunavyoweza kumkataa Mungu katika siku ya leo.

Nyakati Na Majira.

Wakati ufalme wa kusini ulipochukuliwa kuwa mateka hadi Babeli, nyakati mpya ilizaliwa inayojulikana kama 'Nyakati za Watu wa Mataifa'. Mungu alitaka kuwepo na mfumo wa Kithiocracia ambapo Yeye angalikuwa ndiye mfalme nao watu kufanyika watiifu chini ya uongozi wake. Lakini wakati wana wa Israeli walipoukataa huo mfumo, Mungu akasema, 'Sawa basi, nyinyi mtatawanyika katika mataifa,' yaani kwa watu wasio Wakiyahudi, watu wasioamini, 'nanyi mtatawaliwa na watu wa Mataifa.' Kuanzia na kutekwa nyara na Wababeli, Mungu hakuitenda kazi kupitia wafalme kama alivyomtumia mfalme Daudi, ambaye angalitenda mapenzi Yake yote, ila kwa wafalme kama Nebukadreza na Koreshi Mkuu, ambao walikuwa wafalme wa mataifa. Vitabu hivi vya historia kuhusu ufalme vinatueleza kwamba mipango yake Mungu siyo gumu kutekelezwa, kwa kuwa watu wake wanatawaliwa na wafalme wa dunia. Yeye azidi kutimiza mapenzi yake kupitia wao. Nao miradi yake Mungu sio ngumu kutekelezwa wakati tunapomkataa Yeye kuwa ni Mfalme wetu.

Katika 'majira ya watu wa Mataifa', Ufalme wake Mungu upo ndani mwa watu binafsi ambao wamemfanya Mungu kuwa Mfalme wao. Wao huishi miongoni mwa watu wasioamini na kwa wakati mwingi, chini ya utawala wa watu wasioamini. Wao wametawanyika kama chumvi miongoni mwa watu wasioamini ili kuipa ladha dunia. Hii haimaanishi kwamba taifa au nchi ile wanamoishi huwa raia wa Ufalme ni wa Kikristo au wamchao Mungu. Tangu wakati Wayahudi walipoukataa mfumo ambao Mungu aliwatakia *(Theocracia*-utawala chini ya uongozi wake Mungu), hapajakuwepo na taifa ambalo limetawaliwa naye Mungu. Hakuna jambo kama taifa la Wakristo. Ufalme wake Mungu ni ushuhuda ambao uko ndani ya mioyo ya watu binafsi. (Luka 17:9, 10).

Sababu ya nne kufanya marudio yaliyo katika Mambo ya Nyakati ni kwamba hadithi yote haikuwa imeelezwa kikamilifu. Ezra aliamini kwamba waandishi wa vitabu vya Samweli na Wafalme walikuwa wanapasha habari kuhusu nyakati zile katika mtazamo wa kibinadamu hivyo basi, kuliitajika kuwepo mtu ambaye angalitoa historia ile kwa mtazamo wake Mungu. Hii ndiyo sababu yake kuviandika vitabu vya Mambo ya Nyakati 1 na 2.

Mambo Yaliyoachwa.

Hata baada ya historia ile kurudiwa, vitabu hivyo havifanani sana. Tunaweza kupata ishara tofauti katika tafsiri ya Biblia iitwayo *(Septuagint*). Kwa jina lenye kutia mwangaza Mambo ya Nyakati, ambayo yalikuwa: 'Mambo yaliyoachwa.' Jina hili laamaanisha kwamba yapo mambo ambayo hayakunukuliwa wakati historia ile ilipokuwa ikiandikwa katika Samweli na Wafalme na kwamba yapo mambo mengine yaliyojaza kurasa nyingi katika Samweli na Wafalme, kama vile dhambi yake Daudi na Sulemani, ambayo hayakunukuliwa katika Mambo ya Nyakati.

Kutokunukuliwa kwa dhambi yake Daudi ni habari njema. Hili lamaanisha kwamba dhambi zetu huondolewa wakati tunapomjia Mungu kwa kuwa sisi tunamtumainia Kristo kwa ajili ya wokovu wetu. Na kwa sababu ile ile, dhambi yake Sulemani pia haikunukuliwa katika Mambo ya Nyakati zake Ezra.

Siku ya leo, wakati tukio linapojitokeza kwenye runinga (televisheni), wapo wapiga picha kadha mahali pale pa tukio lile. Hivyo basi, ipo sababu vitabu hivi vya Samweli na Wafalme kuitoa ripoti hiyo kwa mtazamo wake mwanadamu na katika Mambo ya Nyakati kupitia mtazamo wake Mungu. Kama vile tunavyoweza kutarajia, baadhi ya 'Yale mambo ambayo hayakunukuliwa' katika Mambo ya Nyakati ni ya kushangaza mno. Kwa mfano, ufalme wa kaskazini wa Israeli, ambao ulikuwa muovu sana, hautajwi baada ya mgawanyiko wa Ufalme. Hii ni kwa sababu gani? Sababu yake ni kuwa kitabu cha Mambo ya Nyakati kinatilia mkazo vizazi vilivyopo katika uzao wake Masiya kwa kuwa yeye angezaliwa kupitia watu wa jamii yake.

Mambo ya Nyakati yanatilia mkazo Wafalme wale waliotumika katika kuleta ufufuo, uhuisho na mabadiliko. Baadhi ya wafalme katika ufalme wa kusini wa Yuda, kama yule Asafu, Yehoshafati, Yoashi, Hezekia, Yosia, walikuwa muhimu sana katika kuleta yaliyo mema. Wafalme waovu (wafalme wote wa ufalme wa kaskazini) hawatajwi kamwe.

Kwa mfano, Yosia, alipanga kwamba Hekalu lipate kufanyiwa marekebisho. Kwa utaratibu huu, Hilkiah Kuhani alizipata hati za nakili ya Maandiko. Watu walikuwa na utovu wa nidhamu na kuasi hivi kwamba wakaisahau kabisa sheria yake Mungu. Hati hizo zilisomwa kwake Yosia, ambaye aligundua mara moja kwamba sheria zake Mungu zilikuwa hazitimizwi, naye akalirudisha taifa kwa Neno lake Mungu (tazama 2 Mambo ya Nyakati 34).

Hivyo basi, kwa mtazamo mwingine, Mambo ya Nyakati yanasaidia katika ufafanusi wa maelezo katika kitabu cha Wafalme. Hii ndiyo sababu katika Wafalme, tunaelezwa mara nyingi kuhusu, 'kushauriana na Mambo ya Nyakati, kushauriana na Mambo ya nyakati,' kwa kuwa mwandishi wa kitabu cha Wafalme (Roho Mtakatifu) anataka sisi kupata mtazamo wa hali ya Mungu kwa mfalme binafsi au kila tukio.

Hebu tumtazame Daudi. Maelezo ambayo yapatikana katika Mambo ya Nyakati kuhusu ufanisi wa kisiasa ni kwa sababu yeye alikuwa amebarikiwa ili kwamba awashirikishe watu wake Mungu katika furaha. Mambo ya Nyakati yatueleza jinsi ambavyo Daudi aliwatayarisha waimbaji na wacheza muziki. Yeye alikuwa na kundi kubwa la wachezaji vinanda vya kila namna na waimbaji wa asili ya Walawi, takribani watu elfu nne. Mchango wake Daudi katika Ibada watiliwa mkazo katika Mambo ya Nyakati ingawaje haukunukuliwa katika vitabu vya Samweli kwa kuwa Mungu anatueleza maana ya ibada kwa maoni yake.

Katika kitabu cha Mambo ya Nyakati vile vile, tunaelezwa sababu yake Daudi kutoruhusiwa kuijenga nyumba yake Mungu. Ilikuwa ni kwa sababu yeye alikuwa mwana vita na alikuwa amemwaga damu nyingi sana. (1 Mambo Ya Nyakati 22:8-9). Ni katika kitabu cha Mambo ya Nyakati ambapo tunapewa maelezo jinsi mfalme mwema kama Yehoshafati alivyoweza kuambatana na mfalme muovu Ahabu – wao walikuwa na wajukuu sawa kwa kuwa wana wao walikuwa wameoana. (2 Mambo Ya Nyakati 18:1).

Ombi la Ufunuo

Aya muhimu sana katika vitabu vya Mambo ya Nyakati inapatikana katika kitabu cha pili cha Mambo ya Nyakati sura ya saba na aya ya kumi na nne:

'Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao.'

Hapa tuna neno kutoka Hekaluni hadi Kasri, kutoka maisha ya kiroho hadi maisha ya kisiasa ya taifa, agano ambalo Mungu aliwapa watu wake. Mungu asema hivi, 'Niko tayari kusamehe, niko tayari kuponya. Lakini kabla yangu kusamehe na kuponya, zipo njia za haki ambazo nahitaji watu wangu kuzipitia.' Naamini kwamba huu ni msitari ambao sote tunahitajika kutia ndani ya mioyo yetu – kwanza, kibinafsi, kisha kwa taifa nzima.

Ufunguo katika kufahamu na kuzikaribisha pamoja tofauti zilizopo na marudio ya wakati huu katika historia ya Kiebrania ni huu: Njia zake Mungu sio njia zetu; mawazo yake sio yetu. Kuna tofauti kuu jinsi ambavyo Mungu hutenda mambo na jinsi ambavyo yeye huyaona mambo, ikilinganishwa na jinsi ambavyo sisi hufikiria na kutenda mambo, kama ilivyo mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi (Isaya 55:8-9). Ikiwa unahitaji kuwa na mtazamo kama ule wa Mungu, na ikiwa unataka kulinganisha jinsi ambavyo unafikiria na kuyatenda mambo, na jinsi ambavyo Mungu hufikiri na kufanya mambo, basi soma kitabu cha Mambo ya Nyakati. Utagundua ujumbe mkuu katika dhamana na mtazamo.

'Mambo ambayo hayakunukuliwa' ni kichwa mwafaka kutumika katika vitabu vya Mambo ya Nyakati. Ni habari njema unapogundua kwamba dhambi zetu hazinukuliwi naye Mungu, jinsi iivyokuwa kwa dhambi zake Sulemani na Daudi kutonukuliwa katika Mambo ya Nyakati. Pia ni changa moto kubwa wakati mtu anapotambua kwamba Mungu hakunukuli ufalme wa kaskazini. Mungu hakutaja ufalme wa kaskazini kwa kuwa raia wenyeji wake hawakuitwa katika kusudi lake Mungu. Na jambo la kushangaza kufahamu kwamba sisi hatutambulikani naye Mungu siku ya leo na katika hali ya milele kwa kuwa mawazo yetu, njia zetu na maisha yetu hayaambatani na mapenzi yake Mungu.

Ni ombi langu kuwa kulinganisha kwako kwa vitabu hivi vya Mambo ya Nyakati na vile vya Samweli na Wafalme kutakupatia changa moto ili kulinganisha mtazamo wake Mungu na ule wa kibinadamu; sio tu wakati huu wa historia bali ni katika wakati huu tunaoishi siku ya leo pamoja na ushiriki wetu katika historia zetu kibinafsi.

SURA YA KUMI

Injili Zinazoabatana Katika Agano La Kale

Katika sura hii, tutaanza kwa kifupi uchuguzi wa vitabu vya Ezra na Nehemia, ambazo pamoja na Esta, vinajulikana kama vitabu vya historia baada ya uvamizi mkuu. Uvamizi wao Wababeli ni ishara ya kuigawanya kwa historia ya Waebrania. Kwa hakika, tunapojifunza kuhusu manabii hapo baadaye, tutagundua kwamba manabii wamegawanywa katika vikundi vitatu: Manabii wa kabla ya Uvamizi, manabii wakati wa uvamizi au Manabii baada ya uvamizi. Ezra, Nehemia, na Esta wananakili wakati huu wa historia hii iliokuwepo na manabii waliokuwa baada ya uvamizi, walipoandika, kuhubiri, kuishi na hata kufariki.

Kurudi Kutoka Utumwa Wa Babeli

Unapoanza kusoma Ezra, Nehemia na Esta, unahitajika kufahamu kwamba kurudi kutoka Babeli kulitokea nyakati tatu tofauti. Kurudi mara ya kwanza kulitokea punde tu wakati Koreshi Mkuu alipoitoa ruhusa. Liwali mkuu Zerubabeli pamoja kuhani mkuu Yoshua waliwaongoza waliorudi mnamo mwaka wa 537 kabla ya kuzaliwa kwake Yesu Kristo. Nia ya kurudi mara ya kwanza ilikuwa ni kulijenga Hekalu. Baada ya kazi kuanza, wale waliokuwa wamerudi waliangaishwa na kufedheheshwa na upinzani pamoja na dhiki, hivyo basi wakaacha ujenzi hadi wakati nabii Hagai na Zekaria walipowatia moyo kumaliza ujenzi huo ambao walikuwa wameanza.

Mnamo mwaka wa 458 kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo, Ezra aliliongoza kundi lingine la pili. Huyu kuhani wa ajabu na mwandishi kitaaluma alikuwa mwalimu mkuu wa maandiko. Ezra aliazisha huduma yenye uwezo ili kulijenga Hekalu. Haya yalitendeka miaka sabini na tisa baada ya kurudi kwa kundi la kwanza na miaka hamsini na nane baada ya ujenzi wa Hekalu kumalizika.

Miaka kumi na tatu baada ya kurudi kwake Ezra, Nehemia aliliongoza kundi la tatu. Nia lake lilikuwa kujenga ukuta uliouzunguka mji wa Yerusalemu. Nabii Malaki alihusika pamoja na Nehemia katika ujenzi wa ukuta huo.

Mambo Yanayofanana Kati Ya Ezra Na Nehemia

Vitabu vya Ezra na Nehemia vinatajwa kuwa ‘vinalingana katika Injili ya Agano la Kale’ kwa kuwa mambo mengi katika vitabu hivyo sawa. Hebu tutazame baadhi ya yale yanaolingana.

- Kwa sababu lugha ya Kiebrania inayotumika katika vitabu hivi viwili inalingana sana, hivyo basi inawezekana kuwa mwandishi wake ni Ezra.

- Wazo kuu katika vitabu hivi viwili ni kuhusu tukio sawa katika historia ya Waebrania: Kurudi kutoka chini ya kongwa ya Wababeli. Wazo kuu katika vitabu hivi viwili ni kazi yake Mungu wakati watu hawa wawili walipokuwa wakiishi: Kati ya kulijenga tena Hekalu Yerusalemu.
- Wote wawili wanatilia mkazo mfumo na kanuni ambazo zilifuatwa ikiwa kazi yake mwanadamu ingalifanyika kuwa Kazi yake Mungu.
- Vitabu hivi vinatupatia mfano bora wa uongozi. Hata ingawa ilikuwa ni mifumo tofauti wa uongozi na karama tofauti, wote walikuwa viongozi wakuu. Ezra alikuwa kuhani na mwandishi, akilifunza neno lake Mungu. Kazi yake Ezra ilikuwa hasa uchungaji. Nehemia alikuwa mtu wa kawaida, mwenye matendo na mjenzi mwenye juhudi.
- Wote wawili waliongoza katika ufufuo wenye upako ambao kwa hakika ulikuwa ni kazi yake Mungu.
- Vitabu vyao vina sadfa: Sura za mwanzo kwa kila kimoja vinanakili orodha ya kazi inayohitajika kutendwa; na baada ya kutimizwa, watu walimuasi Mungu. Na katika Ezra sura ya 9 na Nehemia sura ya 9, tunaona viongozi wote wawili wakiomboleza kwa ajili ya tabia ya watu wao kwa njia ya maombi, huzuni na toba.
- Vitabu vyote viwili vina wafalme wawili wanaopeana ruhusa, wenye huruma, na wenye kuwapa ili kazi yake Mungu ipate kutimizwa kupitia watu Wake.
- Vitu hivi viwili vinamalizika kwa hali ya kutia moyo na yenye matumaini . . .

Somo La Kipekee Kutoka Kwa Ezra

Ingawaje vitabu hivi vya Ezra na Nehemia vinafanana, havina tofauti kuu. Hebu tujifahamishe zaidi kuhusu Ezra.Tunapotilia mkazo kitabu cha Ezra, ni vyema ikiwa tutamtazama kwa makini huyu mtu Ezra. Ezra anahitaji kutajwa pamoja na watu wakuu kama Musa, Samweli, na Daudi. Huduma yake yote ilikuwa ni kuleta mwamko au ufufuo wa kujifunza Neno Lake Mungu.

Katika Ezra 7:10, tunasoma hivi, *'kwa maana Ezra alikuwa <u>ameuelekeza moyo</u> wake kuitafuta sheria ya Bwana, na <u>kuitenda,</u> na <u>kufundisha</u> maagizo na hukumu katika Israeli.'* Msitari huu hauelezi maisha yake yote Ezra, yakiadhimishwa katika nyakati tatu. Theluthi moja ya maisha yake Ezra ilikuwa kujitayarisha kwa theluthi mbili nyingine za maisha yake. Aliuelekeza moyo wake katika kujifunza na kulifahamu Neno lake Mungu, akijifunza kwa bidii. Katika theluthi ya pili, yeye alijitolea kuliishi kulingana na neno lake Mungu, na kutenda yale neno hilo lililosema. Katika theluthi ya tatu ya

maisha yake, Ezra alijitolea kabisa kulifunza neno lake Mungu na kuwafanya wanafunzi baadhi ya katika njia zake Mungu.

Hii ni njia bora ya kuishi maisha yako. Nafikiri kwamba shida moja iliyopo katika kufundisha siku ya leo ni kwamba tunao watu ambao hujitayarisha na kufundisha, lakini wao waweza kuifundisha elimu ya maarifa tu. Wao hawawezi kufunza kutoka akiba ya ujuzi wao. Mwalimu aliye bora ni mtu yule ambaye ametumia theluthi ya pili ya maisha yake kupata ujuzi aliojifunza katika theluthi ya kwanza ya maisha yake. Baada ya ujuzi, theluthi ya mwisho ya maisha yake inaweza kutumika kwa faida kuu kwa kufundisha.

Unapokadiria mchango wake Ezra katika kazi yake Mungu, unaweza kuona sababu yake kuwa katika cheo kimoja sawa na Daudi, Samweli na Musa. Jinsi nilivyotaja hapo awali, Ezra atambulikana kama mwandishi wa vitabu vya Mambo ya Nyakati, Ezra, na Nehemia, na kwamba yeye pia aliandika sura iliyo ndefu mno katika Biblia, Zaburi 119, ambayo ina aya au misitari 176. Zaburi hiyo moja ni ndefu kuliko baadhi ya vitabu vingine katika Biblia. Katika misitari hii 176, kila msitari isipokuwa miwili peke yake inataja maandiko. Hii inaonyesha jinsi huyu Ezra alivyokuwa amejitolea kwa neno lake Bwana.

Kulingana na historia, wasomi wanaamini kwamba wakati Ezra alipokuwa uhamishoni kama mateka hangeliitenda kazi yake kama kuhani ndani ya Hekalu. Kwa hivyo, yeye alibuni kile tunachofahamu kama Sinagogi, inayolinganishwa na Shule ya Jumapili siku hizi. Wasomi pia wanaamini kwamba Ezra alihusika sana katika harakati za kuandaa Agano la Kale jinsi ilivyo siku ya leo. Pamoja na mchango wake, yeye pia aliliongoza kundi la pili kurudi kutoka utumwa wa Babeli. Ilikuwa ni Ezra mwenye kuibuni huduma thabiti ya kufundisha ndani ya Hekalu, ambalo lilikuwa limejengwa kabla ya kurudi kwake kutoka uhamishoni. Yeye aliwarudisha baadhi ya wahudumu miongoni mwao wakiwepo makuhani na waandishi waliowafundisha watu Neno lake Mungu pamoja naye baada ya kurudi kwao.

Kanuni Pamoja Na Mfumo Wa Kazi Ya Mungu

Kitabu cha Ezra kinatupatia mafunzo kuhusu kazi yake Mungu – Kanuni ambazo pia ni mfumo kwa kazi yake. Kanuni ya kwanza ni kuwa: wakati kazi yake Mungu inapotakikana kutendwa, Mungu, Mwenyewe ndiye kinara mikuu wa uongozi wa kazi yake (linganisha na Warumi 11:36). Mungu ndiye kina kikuu cha kazi hiyo, ndiye nguvu iliyo nyuma ya kazi ile, na utukufu wake ndiyo

kusudi la kazi hiyo. Naamini kwamba hii ndiyo njia ambayo huyu Ezra aliambatanisha na kuipa dhamana kuu katika huduma ya maisha yake, yenye msingi katika msitari wa kwanza wa kitabu hiki.

Kanuni ya pili tunayojifunza kutoka kwake Ezra ni hii: Wakati Mungu, Kinara mkuu, anapotaka kutimiza mapenzi yake kupitia watu, yeye huwapa watu maongozi dhahiri na hasa vyombo vya kibinadamu ambavyo wataitekeleza ile kazi kwa niaba yake.

La tatu: Mungu ambaye ndiye Kinara mkuu ambaye ndiye hufanya dhahiri mwongozo wake, atatoa kila kitu kinachohitajika ili kuona kwamba kazi yake imetimizwa. Hii ni kanuni muhimu sana, ambayo inatajwa mara nyingi katika maandiko. Katika Mathayo 6:33, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, *'Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazindishiwa.'* Tunapofahamu kile ambacho Mungu anahitaji sisi kutenda, nasi tunapotenda yale yaliyo sawa mbele ya macho yake, Yeye atatuzidishia yale yote tunayohitaji ili kutimiza kazi yake.

Kanuni ya nne ni kuwa: Wakati Mungu anapotaka kuitekeleza kazi yake, Yeye atatoa sio tu kile kinachohitajika, bali pia kupita kile tuombacho, au hata kukifikiria kukiomba (tazama Waefeso 3:20). Katika kazi au huduma yake Ezra, wale waliorudi walikuwa na uwezo mdogo wa kuitimiza ile kazi; lakini wao walikuwa na zaidi ya kile kilichohitajika kulijenga Hekalu.

Kanuni ya tano: Unapofanya kazi yake Mungu, tarajia Shetani kuipinga kazi yake Mungu njema, kwa yale yaonekanayo kuwa mazuri. Adui wetu atajaribu kutuhangaisha sisi ili tusiitende kazi bora kwake Mungu kwa kutunong'onezea hivi, 'Timiza jambo lile lililo nzuri, lakini usijaribu kutekeleza mpango bora wake Mungu kwa maisha yako.'

Tutaitazama hii kanuni ya tano kwa makini zaidi, pamoja na zingine za ziada katika sura ifuatayo.

SURA YA KUMI NA MOJA.

Nguvu Za Kupinga Kazi Yake Mungu.

Kanuni ya tano tuliyoitazama katika kitabu cha Ezra ilikuwa ni: Tunapojiandaa kuitekeleza kazi yake Mungu, nguvu za uovu katika ulimwengu huu huleta upinzani kwetu. Tunahitajika kusoma hila zake Shetani kwa undani ili tuweze kufahamu yale Ezra pamoja na Wayahudi waliorudi kutoka Babeli waliyokubana nayo.

Mtume Paulo atuhimiza kuzifahamu hila zake shetani. (tazama 2 Wakorintho 2:11; 10:3-5; 11:13-15). Shetani ni mwenye hila. Apenda kuiga na kudanganya. Yeye anafahamu kwamba adui mkuu wa yaliyo bora zaidi ni bora. Wakati Mungu anapofanya kazi kukupitia wewe, utaupata ujuzi bora kutoka kwake Mungu. Ni kwa sababu Shetani ni mjanja, yeye afahamu kuwa hawezi kufanikiwa kukuhangaisha wewe kwa kutotenda yaliyo bora kwake Mungu, kwa kukufanya wewe kuwa jambazi la kuvunja benki. Yale atakayofanya ni kukuhadaa ili ulitende jambo lililo nzuri tu. Ikiwa wewe unaishi kwa utajiri, na faraja nyingi na yaliyo bora kutoka kwake Mungu kwako ni jukumu lako wewe kufanyika kuwa Mmishionari daktari pale ambapo hamna usaidizi wa kimatibabu kwa watu wa jamaa fulani. Shetani atakujaribu wewe ili ufanyike kuwa daktari mwema mahali ulipo. Hili linaweza kuwa lengo kuu katika maisha yako, lakini hii ni dhamana ya chini kuliko lililo bora zaidi ambalo Mungu akutakia wewe kuwa ni Mmishionari daktari kwa watu wenye mahitaji katika mazingara magumu.

Kanuni ya sita ambayo Ezra anatueleza sisi inaambatana kwa karibu sana na ile iliyotangulia: Wakati wote tarajia upinzani unapojaribu kuitekeleza kazi yake Mungu. Wakati watu wanapojitayarisha kuitekeleza kazi yake Mungu na punde tu wanapokubana na upinzani, wao hupata mashaka ikiwa yale wanayotenda ni kazi yake Mungu. Hili kwa hakika si kweli! Mungu hutenda kazi kupitia watu, na vivyo hivyo Shetani pia huwatumia watu. Kwa sababu Shetani ni mpinzani wa kila kitu ambacho Yesu Kristo anafanya, tunahitajika kutarajia upinzani wakati Kristo anapoitenda kazi kutupitia sisi. Wakati mwingine watu wenye kutupa upinzani hawatambui kwamba wao ni mabalozi wake shetani (linganisha na Marko 8:27-33).

Kitabu cha Ezra kinatujulisha kwamba upinzani utatujia kutoka pande mbili. Kwanza, kutakuwa na upinzani wa kawaida kutoka nje. Kutakuwepo kila mara hapa ulimwenguni watu ambao hawatatutakia heri tunapojitayarisha kuitekeleza kazi yake Mungu. Kwa mfano, wakati hawa mateka waliporudi Yerusalemu ili kulijenga Hekalu, watu waliokuwemo huko walijaribu kuwavunja moyo na kuwatia hofu. Wao walituma ujumbe wa uongo kwake mfalme Artashasta. Nao watu wake Mungu ikawalazimu kuisimamisha kazi yao ya ujenzi. (Ezra 4). Kitabu cha Nehemia pia kinasema kwamba wakati wao walipokuwa wakijenga kuta, walikuwa na vyombo vya ujenzi mkononi mmoja na silaha

kwenye mkono ule mwingine. (Nehemia 4:17) na kwa mtazamo mwingine, upinzani utoka nje na ni mwepesi kukubana nao kwa kuwa ni dhahiri–upo huko nje ambapo sisi tunaweza kuona na kupigana nao.

Upinzani wa namna ya pili ni ule utokao miongoni mwetu. Wakati hawa mateka waliporudi ili kulijenga Hekalu, watu wa Mataifa waliokuwa wakiishi Yerusalemu na Uyahudi walimwendea Zerubabeli na Yoshua na kusema, *'Wakamkaribia Zerubabeli, na wakuu wa mbari za mababa, wakawaambia, Na tujenge sisi nasi pamoja nanyi; kwa maana tunamtafuta Mungu wenu kama ninyi; kwa maana tunamtafuta Mungu wenu kama ninyi, nasi twamtolea dhabihu tangu zamani za Esar-hadoni, mfalme wa Ashuru, aliyetupandisha mpaka hapa.'* (Ezra 4:2). *Lakini Zerubabeli, na Yoshua, na wakuu wengine wa mbari za mababa katika Israeli, wakawaambia, Ninyi haiwahusu kushirikiana nasi katika kumjengea Mungu wetu nyumba; bali sisi wenyewe peke yetu tutamjengea Bwana, Mungu wa Israeli, nyumba, kama mfalme Koreshi, mfalme wa Uajemi, alivyotuamuru.* (3). Zerubabeli na Yoshua walithibitisha kanuni hizi kuhusu kazi yake Mungu: Ni lazima ifanywe na watu wake Mungu. Hapo ipo njia ya kuyanena maneno haya kwa usemi tofauti:

Ni mpango wake Mungu

Kuzitumia nguvu zake Mungu

Kupitia watu wake Mungu

Kuyatimiza makusudio yake Mungu

Kulingana na mpango wake Mungu.

Kazi ya Mungu yatakikana kufanywa na watu wake Mungu. Wasioamini hawana fursa ye yote ile. Naamini kwamba unyonge mmoja uliopo katika Kanisa siku ya leo unatoka kwa kweli kwamba kuna mchanganyiko wa umati wa waumini pamoja na wasioamini. Makanisa mengi yanawachukua viongozi katika jamii, watu wenye sifa, mali, na wenye kutambulikana–bila kujali kana kwamba wao ni waumini au hapana. Lakini kazi yake Mungu lazima ifanywe na watu wake Mungu, sio tu mtu ye yote yule anayetaka kufanyika kuwa sehemu yake kwa kuwa ni jambo njema au shughuli inayokubalika kijamii. Hebu fikiria mtu katika moja ya taaluma ambazo ni muhimu kwake kukutana na watu wengi–(Daktari wa meno, ambaye hamwamini Yesu Kristo, ni mfano bora kwake yeye anayekutana na jamii zenye watoto.) Yeye angelitaka kufanyika kuwa mkuu wa shule ya Jumapili katika Kanisa kubwa mjini ili akutane na jamii hizo. Hilo litakuwa

jambo nyepesi sana kutenda kwa kuwa Kanisa la kawaida lipo po pote pale lingemkaribisha yeye. Lakini hata hivyo, jambo hili litavunja kanuni hii ambayo tunajifunza katika kitabu cha Ezra kuhusu kazi yake Mungu.

Kanuni ya saba ni kuwa: Mungu ambaye ndiye kiongozi mkuu, anayetoa uongozi dhahiri, na ambaye hukutana na mahitaji yote yale yanayohitajika kwa kazi Yake, atautoa ushindi ili kukumbana na upinzani wa kazi Yake. Kanuni hii yenye kuvutia sana yahitajika kututia moyo na kutupatia tumaini kwa watumishi wake Mungu ambao wanakumbana na upinzani kote katika ulimwengu.

Mungu yule yule wa Ezra na Nehemia ana uwezo wakushinda upinzani katika kazi Yake siku ya leo kama ilivyokuwa siku yao. (tilia maanani Ezra 6:6-8). Ujumbe ulikuwa umetumwa kwake mfalme Artashasta, ukiwashitaki kwamba Wayahudi walikuwa waasi na wenye historia ya kuasi; hivyo basi, wasipewe ruhusa kulijenga hekalu lao (Ezra 4:11-16). Lakini wakati mfalme aliyekuja baadaye alipokuwa akitafuta katika mambo ya nyakati ya ufalme huo, aligundua kwamba Koreshi Mkuu alikuwa kwa hakika ameitoa amri na kufanya matoleo ili Hekalu lipate kujengwa upya. Baadaye aliandika haya:

'Iacheni kazi hii ya nyumba ya Mungu, msiizuie; waacheni liwali wa Wayahudi, na wazee wa Wayahudi, waijenge nyumba hii ya Mungu mahali pake. Tena, natoa amri kuwaagiza nyinyi mtakayowatendea wazee hao wa Wayahudi, kwa kazi hii ya kuijenga nyumba ya Mungu; katika mali ya mfalme, yaani, katika kodi za nchi iliyo ng'ambo ya Mto, watu hao wapewe gharama zote kwa bidii, ili wasizuiliwe.' (Ezra 6:7-8).

Mungu aliushinda huo upinzani. Mapenzi yake pamoja na kazi yake yalitimilizwa.

Kanuni ya nane ni hili: Kama ilivyo Mungu huitenda kazi yake kupitia watu Wake, watu wa Mataifa wenye kutazama wataokolewa huku wakiitazama kazi hiyo ya Mungu. Wakati watu wanapomwona Mungu akitenda kazi kutupitia sisi, wakifahamu kwamba sisi ni vyombo vya udongo ambavyo havingetimiza lo lote peke yetu, wao huanza kutambua kwamba hii ni kazi yake Mungu. Wao huanza kutambua kwamba Mungu ndiye kiongozi mkuu, kina, na ndiye uwezo ulio po pote pale watu wake wanaitenda kazi yake.

Hivi ndivyo watu huokolewa wakati wanapoitazama kazi yake Mungu. Katika Ezra 6:21-22, tunasoma kwamba baadhi ya watu wa Mataifa ambao walikuwa wamehamishwa na kuletwa huko Yuda waligeuka na kuziacha mila zao za dhambi na kuungana katika kumwabudu Bwana Mungu wakati Wayahudi wote waliposhiriki katika sherehe ya Pasaka. Hii ni tofauti na wasioamini ambao wanataka kuhusika katika huduma au kazi yake Mungu badala ya kuzaliwa kwa mara ya pili. Wakati watu wa Mataifa wanapookolewa, wao hufanyika kuwa sehemu ya watu wake Mungu na pia hufanyika kuwa watu ambao Mungu hutaka kuifanya kazi yake kuwapitia katika ulimwengu huu.

Sasa tunaingia katika kanuni ya tisa: wale wote ambao wanahusika katika uongozi wa kazi yake Mungu wataipata kazi hiyo kuwa imedhihirishwa katika Neno lake Mungu. Hapa Ezra hufanyika kuwa mfano kwetu sisi. Ezra alikuwa ameazimia ndani ya moyo wake kujifunza neno lake Mungu. Aliifahamu kazi yake Mungu ilikuwa ipi kwa kuwa alilifahamu Neno lake. Nayo kazi ambayo Mungu alikuwa nayo kwake Ezra ilikuwa ni kuthibitisha huduma yenye mafundisho ya uweza mkuu katika Hekalu lililojengwa upya.

Kanuni ya kumi ni dhahiri mno: Wakati kazi yake Mungu inapokamilishwa, Mungu huwaruhusu watu wake kushindwa ili kwamba iwe dhahiri kwa watu wote

kwamba uwezo na nguvu zote zilikuwa kutoka kwake Mungu peke yake. Katika vitabu vya Ezra na Nehemia, baada ya kazi ile kuu kutimizwa, watu walirudi nyuma. Watu wake Mungu walijikuta katika desturi mbovu za watu wa Mataifa waliokuwa miongoni mwao katika nchi hiyo. Hili ni jambo la kuhuzunisha na tukio lenye kutiliwa maanani kwa watu wengi wakuu na huduma zake Mungu. Inawezekana kwamba Mungu hutaka kutuonyesha sisi na ulimwengu wote kwamba ni Yeye mwenyewe aliye kina cha kazi yake na wala sio wanadamu ambao ni vyombo vya kazi yake.

Kuna sababu nyingine ya matukio haya, ambayo yanahusu Shetani. Kanuni ya kumi na mmoja: Wakati Mungu ameifanya kazi yake kupitia mtu ili kutimiza kazi yake, Shetani hupenda kukejeli vyombo vya kibinadamu ambavyo Mungu huvitumia ili kuifanya kazi yake.

Hizi ni baadhi ya kanuni kuhusu kazi yake Mungu ambazo tunajifunza katika kitabu cha Ezra. Kumalizia kwa kutilia mkazo, nayarudia haya Ezra anayotueleza: **Ni mpango wake Mungu kutumia nguvu zake kupitia watu wake kutimiza nia yake kulingana na mpango wake.**

Je, wewe ni mmoja wa watu wa Mungu? Je, wewe unafahamu kwamba u chombo cha uwezo wake Mungu? Je, unafahamu nia ya nguvu zake Mungu ndani yako ili kazi yake ipate kutimizwa kupitia wewe, kulingana na mpango Wake?

SURA YA KUMI NA MBILI

Sifa Za Kiongozi

Mahali ambapo kitabu cha Ezra kinapotuonyesha kanuni za kuhakikisha kwamba kazi yetu kwake Mungu itakuwa ni kazi yake Mungu, kitabu cha Nehemia kinatilia mkazo juu ya kiongozi, namna ya kiongozi wa kibinadamu ambaye Mungu anatafuta ikiwa ataitenda kazi yake kupitia watu. Nehemia mwenyewe ni mfano wa kiongozi huyo.

Wakati Nehemia alipokuwa liwali mkuu, watu walihitaji uamsho. Wengi wa Wayahudi walikuwa wameoa watu wa Mataifa waliowazunguka, kinyume cha sheria Yake Mungu. Hebu sikia maonyo yake Nehemia: *'Tena siku zizo hizo nikawaona wale Wayahudi waliokuwa wameoa wanawake wa Ashdodi, na Amoni, na Moabu; na watoto wao wakanena nusu kwa lugha ya Ashdodi, wala hawakuweza kunena kwa Kiyahudi, bali kwa lugha ya watu hao mojawapo. Nikagombona nao, nikawalaani, nikawapiga baadhi yao, na kuwang'oa nywele zao; nikawaapisha kwa Mungu, nikasema, Msiwaoze wana wao binti zenu, wala msiwatwae binti zao ili waolewe na wana wenu, wala na nyinyi wenyewe.'* (Nehemia 13:23-25).

Unaweza kuona kwamba Nehemia alikuwa na mfumo tofauti wa uongozi! Sio wengi miongoni mwa wachungaji walio na uongozi wa namna hii, lakini Nehemia alikuwa hivyo kwa kuwa hivi ndivyo watu wake Mungu walivyohitaji kuwa wakati huo.

Tunaweza kusema kwamba Ezra aliandika au kuunda mfumo kwa kazi yake Mungu, ilhali huyu Nehemia alikuwa mjenzi ambaye kwa hakika alifanya kazi yake Mungu waliyokuwa wamepewa. Neno kwake Nehemia ni dhahiri na linaweza kutendeka. Yeye aliamini kutoka huko nje, kuona na kuhakikisha kwamba ile kazi imetendeka. Hawa watu wawili ni mifano mwafaka kabisa kuhusu uongozi, ingawaje wao walikuwa kuwa watu tofauti.

Tunapokaribia kitabu cha Nehemia, tunahitajika kutazama kanuni za viongozi, au tabia ambazo Mungu alizipata ili kuitenda kazi yake. Ninakiita kitabu chake Nehemia: 'Tabia ya kiongozi wa kazi yake Mungu.'

Ishara ya tabia ya kwanza ambayo Nehemia alidhihirisha ni kuwa: mzigo wa kazi ambayo Mungu ataka kutenda. Ishara ya kwanza ambayo inaonyesha kwamba Mungu ataka kuitenda kazi ile kupitia wewe ni kwamba unausikia mzigo wa ile kazi. Ikiwa unahusikia ule mzigo na unaomba kuhusu, Mungu anaweza kukuhitaji wewe kuwa sehemu ya jibu la maombi yako.

Ishara ya pili ni kuwa: Mtu mwenye kuongoza kazi yake Mungu ni lazima awe na neno kutoka kwake Mungu kuhusu kazi ile. Katika Nehemia 1:9, Nehemia alikumbuka Neno lake Mungu kwake Musa: *'bali mkinirudia mimi, na kuzishika amri zangu na kuzitenda, watu wako waliofukuzwa wajapokuwa katika pande za mwisho za mbingu, hata hivyo nitawakusanya kutoka huko, na kuwaleta mpaka mahali pale nilipopachagua ili kuliweka jina langu hapo.'* Mahali hapo palikuwa ni Yerusalemu. Mungu alimtaka Nehemia kujenga ukuta uliozunguka mji wa Yerusalemu.

Ishara ya tatu ni: kujitolea kwa kazi ambayo Mungu anataka kuitekeleza. Mtu yule awe ni mume au mke ambaye Mungu humpata ili kuitekeleza kazi yake sio kuwepo na mzigo na kuwa na neno kutoka kwake Bwana, bali lazima pia wawe na kujitolea kwa Bwana kuitimiza kazi yake Mungu. Kujitolea kwake Nehemia kwa kazi yake Mungu kunaonekana kwa kujitolea katika wajibu wake kama mfalme. Ilikuwa ni sheria ya Mede-Uajemi kwamba, kama ulikuwa mwenye huzuni au mwenye nia mbaya mbele yake mfalme, ungekuua. Hata hivyo, katika Nehemia 2:2, tunasoma kwamba mfalme alimwuliza Nehemia hivi, '*Mbona umesikitika uso wako?'* Nehemia anatueleza kwamba yeye alijawa na woga na kuomba kimoyo-moyo Mungu wa mbinguni. Hata hivyo, akamweleza mfalme yale yaliyokuwepo moyoni mwake. *'Mfalme na aishi milele; kwani uso wangu usiwe na huzuni, iwapo mji, ulio mahali pa makaburi ya baba zangu, unakaa ukiwa, na malango yake yameteketezwa kwa moto? (*3).' Bwana alikuwa naye Nehemia kwa kuwa mfalme aliuliza hivi, *'Una haja gani unayotaka kuniomba?* (4).' Huku akimwomba Mungu wa mbinguni, Nehemia alimwambia kwamba yeye angelipenda kurudi huko Yerusalemu na kuili auebdee mji wa makaburi ya baba zake, apate kuujenga (5). Bali na mfalme huyo kuyakubali maombi yake, pia alimpatia yale yote aliyohitaji. Mungu alimbariki Nehemia kwa kujitolea kwake katika kazi Yake.

Ishara ya nne ni: maono kwa kazi yake Mungu. *'Pasipo maono, watu huacha kujizui.'* (Mithali 29:18). Kiongozi wa kazi yake Mungu anahitajika kuwa na maono na ni lazima awashirikishe wengine. Nehemia aliporudi huko Yerusalemu, alifanya uchuguzi wa siri kuhusu uharibifu uliokuwepo katika mji ule na makadirio yaliyohitajika. Baadaye aliambatana na makuhani, wazee na viongozi

wengine huku akiwaambia, *'Haya! Na tuujenge tena ukuta wa Yerusalemu* (17).' Wakati alipofahamu kile alichohitaji kutenda, hapo ndipo alipowaeleza wale wengine.

Ishara ya tano yake ni: kuwahuzisha wengine katika kazi ile. Wakati kiongozi anapopata maono kutoka kwa Mungu, yeye huwashirikisha wengine katika maono yale, nao watu wake Mungu wataufuata uongozi wake. Wakati mwingine, viongozi wa kiroho hukata tamaa kwamba watu wake Mungu hawatawafuata. Lakini wao pamoja nasi tunahitajika kutambua kwamba kupungukiwa na 'wale ambao wako tayari kutufuata' huonyesha upungufu katika uongozi wetu, kwa kuwa mojawapoya tabia au sifa za kiongozi wake Mungu ni uwezo wa kuwahimiza watu kuwafuata wao katika kuitenda kazi yake Mungu.

Ishara ya sita na ya uthibitisho wake kiongozi mwenye upako wa Roho Mtakatifu ni kuwa na wapinzani. Unapoanza kutenda jambo fulani, na hasa kazi yake Mungu, unaweza kutarajia upinzani na kukosolewa–hata kutoka kwa watakatifu na watu wa kiroho. Nehemia alikuwa na uthibitisho kutoka kwa wapinzani wake (4:1-3).

Ishara nyingine ya saba ni maisha ya maombi yenye kina chake katika kazi yake Mungu. Hebu tazama idadi ya nyakati ambazo huyu Nehemia anazitaja kwetu kuhusu kuomba kwake. Nehemia alifanya maombi wakati watu walimdhihaki na kumchekelea (4:4-5). Pia aliomba kabla ya kuzungumza naye mfalme (2:4). Yeye atuonyesha maana ya kutumia maonyo yake Paulo yaani, 'Ombeni bila kukoma.' (1 Wathesalonike 5:17).

Ishara au sifa ya nane ya kiongozi wake Mungu ni kuwa pamoja na watu wakati wanapoitenda kazi. Nehemia alikuwa kwenye kuta zile pamoja na wote waliohusika.

Ishara ya tisa ni chuki ya kitaua kinyume cha upinzani na pingamizi kwa kazi yake Mungu. Kuna tofauti gani kati ya chuki tauwa na hasira? Ikiwa wewe umekasirika kwa sababu ya kitu fulani au mtu fulani kuwa ameifunga nia yako, nawe umetilia maanani kwamba lazima ufanye kile ambacho umekusudia, hasira ile ni dhambi. Lakini kama waifanya kazi yake Mungu nawe ukasirikie nguvu za kuzimu ambazo zinaleta viunzi kwenye njia zake Mungu, hakika hasira yako ni haki. Kwa mfano, wakati Yesu alipoona kwamba uongozi wa kidini ulikuwa umeifanya nyumba yake Mungu kuwa soko la biashara na pango la wezi, hapa alidhihirisha hasira ya haki. (tazama 2:12-16).

Kiongozi wa kazi ya Mungu aweza kuwa na hasira ya haki wakati anapokumbana na pingamizi katika kazi yake hiyo. Naye Nehemia alikuwa kiongozi wa aina hiyo.

Sifa ya kumi ni kujitolea kabisa kwa kazi yake Mungu. Hebu tazama mistari iliyo katika Nehemia 4:21-23.

'Hivyo tukajitia katika kazi hiyo; na nusu yao waliishika mikuki, tangu alfajiri hata nyota zikatokea. Kadhalika, wakati ule ule, nikawaambia watu, Kila mtu na akae ndani ya Yerusalemu pamoja na mtumishi wake, wapate kuwa walinzi wetu wakati wa usiku, na kufanya kazi wakati wa mchana. Basi mimi, na ndugu zangu, na watumishi wangu, na watu wa ulinzi walionifuata, hatukuvua nguo zetu hata mmoja; kila mtu alikwenda kuteka maji akichukua silaha yake.' Huu ni mfano bora insi ya kujitolea kwa kazi yake Mungu.

Sifa ya kumi na moja kwa kushangaza kabisa ni kuwa na maono yaliyo kama bomba. Maono kama bomba yanaweza kuwa mema au mazuri. Yatakuwa mabaya wakati unapokuwa shingo ngumu na unapokataa kusikiza mashauri. Lakini yatafanyika kuwa mema wakati yatakapofanya sisi kutokuwa na nia mbili katika kazi yake Mungu. Watu wengi walijaribu kwa hila mbali mbali kumwondoa yeye katika kazi ya Mungu. Lakini hawangelimfikia huyu Nehemia katika ujenzi wa kuta alizokuwa akizijenga. Watu wengi walitumia ujanja mwingi ili kumfanya ashuke chini katika ujenzi, lakini hawakumfanya kusita-sita katika huduma ile kwa kuwa alikuwa amelenga shabaha yake kwa kazi ya Mungu.

Ishara ya kumi na mbili ni kushawishika kwa dhati. Katika sura ya 5, wakati Nehemia anapotambua kwamba baadhi ya watu wanahujumu ndugu zao kwa kuwatoza riba, yeye anawalazimisha wao kukubali kwamba hawatawahujumu jamaa zao wa Kiyahudi (1-13). Nehemia alikuwa mtu mwenye ushawishi mwingi.

Ishara ya kumi na tatu ni ujasiri mkuu. Nehemia alifahamu kwamba alikuwa akitenda kazi kuu naye alikuwa na uhakika thabiti kwamba Mungu alikuwa amemwita kwa kazi ile. Jambo hili lilimpa Nehemia ujasiri usio na kipimo alipokuwa akitenda kazi ile ambayo Mungu alikuwa amempa.

Ishara ya kumi na nne ya ni kuwa shujaa asiye na woga. Ushujaa ni sifa muhimu sana ya kiongozi ambaye Mungu anaweza kumtumia.

Ishara ya kumi na tano ni subira. Katika Warumi 5, mtume Paulo anatupatia mwangaza jinsi subira hukuzwa na kuendelezwa: *'Wala si hivyo tu, ila na mtufurahi katika dhiki pia; mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi; na uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini; na tumaini halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi* (3-5).' Subira inamaanisha kukaa pamoja na kitu bila kukata tamaa-hata katika dhiki, sisi huvumilia.

Ishara ya kumi na sita ni usanifu katika jinsi ya uongozi. Maandiko yanaeleza mfumo dhahiri wa kufanya kazi yake Mungu katika Kanisa. (linganisha 1 Wakorintho 12:28, hasa kile kipawa cha uongozi). Katika Nehemia 7, Nehemia aliwachagua Walawi, wazee pamoja na walinzi. Pia aliwaandikisha watu kulingana na jamii zao. Hii ni jinsi ya usanifu katika uongozi!

Ishara ya kumi na nane ni kutilia mkazo lengo la dhamana kuu. Tazama dhamana za Nehemia katika sura ya 10. Aliwafanya watu kukubaliana kwamba wao hawatawaruhusu wana wao kuolewa na watu wa Mataifa, kwamba hawataifanya kazi siku ya Sabato, na kwamba hawatailima ardhi yao kila baada ya miaka saba. Alitilia mkazo kwamba wao walipe ushuru wa Hekalu, watoe mavuno ya kwanza kwake Mungu, na kuwatoa wazaliwa wao wa kwanza na wale wa wanyama wao kwake Mungu. Watu wake Mungu walimwahidi Nehemia kwamba wangalimpa Mungu sehemu ya kumi ya yote waliokuwa nayo. Nehemia alizifahamu dhamana zake, naye aliwaongoza watu kukubaliana na dhamana zake.

Sifa ya kumi na nane ni kuongoza kwa fimbo ile ya mchungaji. Jinsi alivyo mchungaji mwema, kiongozi huitumia fimbo yake mchungaji katika kuongoza na kuwapa nidhamu watu wake Mungu. Jinsi alivyo mzazi mwema, kiongozi lazima awapende watu wake vyakutosha ili kuwapa nidhamu wao.

Ishara ya kumi na tisa ya ni kwamba kiongozi ana uhusiano na utu wake wa kibinadamu. Kiongozi ni mwanadamu na anastahili afahamu hivyo. Sio kwamba yeye ana uhusiano pamoja na utu wake wa kibinadamu tu, bali hata pamoja na utu wa kibinadamu wa watu ambao anawaongoza.

Mwishowe, Nehemia anatuonyesha ishara ya ishirini ya kiongozi wake Mungu, ambayo ni kuikamilisha kazi ambayo Mungu amemwajibisha kwake kwa utukufu wake Mungu. Nehemia aliukamilisha ujenzi wa kuta za Yerusalemu kwa utukufu wake Mungu! Tunahitajika tusipoteze shabaha yetu ya kukamilisha huku tunapotijahidi katika kazi ambayo Mungu anataka kutenda kutupitia sisi. Kiongozi wake Mungu ni mtu ambaye anaweza kusema maneno haya pamoja na Yesu, *'Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye…..Imekwisha.'* (soma Yohana 17:4; 19:30).

SURA YA KUMI NA TATU.

Hebu Kisia Ni Nani Atakayekuja Kwa Chakula Cha Jioni!

Agano la Kale linanakili ukombozi mkuu kwa mara nne kuhusu watu wake Mungu. Ukombozi wa kwanza waja kupitia Yusufu, ambaye aliwakomboa Waebrania kutoka janga kuu la njaa na ukosefu wa vyakula. Wa pili ni–ukombozi wa Israeli kutoka utumwani na mateso ya kimabavu huko Misri. Ilhali wa tatu ni kurudi kwa Wayahudi kutoka utumwani huko Babeli. Hatimaye, wa mwisho ni ule ambao unanakiliwa katika kitabu cha Esta.

Vitabu vya Ruthu na Esta ni nakala kuhusu wanawake wenye tabia za kuvutia ambao walifanya tofauti kuu na kuchangia katika kazi yake Mungu. Ruthu anatueleza kuhusu mwanamke wa kimataifa ambaye aliolewa na Myahudi na kufanyika sehemu ya nisaba yake Masiya. Esta anatuambia hadithi ya mwanamke wa asili ya Waebrania ambaye aliolewa na mtu wa Mataifa na kuwaokoa watu wa Kiyahudi kutokana na mauaji makubwa, na hivyo kuhifadhi nisaba yake Masiya. Kwa sababu kitabu hiki ni maelezo ya hadithi yake kama mchezo wa kuigiza, nitaufanya ukachuguzi wangu kuhusu kitabu hiki cha Esta kana kwamba ni mchezo wa kuigiza.

ONYESHO LA KWANZA.

Mipango Ya Watu

Sehemu Ya 1: Karamu Ya Uajemi.

Ni mwaka wa 482 kabla ya kuzaliwa Yesu Kristo na maandalizi ya karamu hii ya Uiajemi ni katika jimbo la 127 ilioko Mede- Uajemi, ambayo ni katika Milki ya Uajemi. Mhusika mkuu ni malkia aliyeondolewa, malkia Vashti. Mumewe ni mfalme Artashasta, au Ahasuero (kulingana na tafsiri zingine za Biblia). Karamu hii ilikuwa ni ya muda wa miezi sita na juma moja, na kinywaji kiliandaliwa vilivyo. Kikwazo kilichokuwepo ni kuwa kunywa kulikuwa kama ilivyoamriwa, bila sharti, maana ndivyo mfalme alivyowaagiza watumishi-wa-nyumbani (Esta 1:8).

Malkia Vashti aliwatumbuiza wanawake mbali pamoja na wanaume. Lakini shida ilitokea wakati alipoitwa naye mfalme mumewe aje na kuonyesha urembo wake mbele za wanaume ambao walikuwa walevi chakari kwa kileo cha muda wa miezi sita na juma moja. Yamkini unaweza kutambua ni kwa sababu gani yeye alikataa kuja mbele ya mfalme. Na kwa nia mbaya, mfalme Artashasta au Ahusuero hakuielewa jambo hilo kamwe.

Sehemu Ya 2: Kutimuliwa Mamlakani Kwake Malkia Vashti

Washauri wake Ahasuero walimshauri yule mfalme mwenye kughadhibika na hasira kwamba tabia yake Malkia Vashti iliwashusha daraja waume wote katika milki yote. Na kwa sababu yeye alikataa kimtii yeye, wake zao pia wangelikataa na kuwadharau machani pao. Hivyo basi, wakamshauri mfalme kumng'oa mamlakani Malkia Vashti na kumtafuta malkia mwingine, mwenye kufaa (na aliye msikivu). Hivyo basi, wakati wake wengine watakapoyaona haya yaliyotendeka kwake Vashti, wao watawaheshimu waume zao. (16-20).

Mfalme Ahasuero pamoja na akida wake wote waliona kwamba jambo hili ni la kufaa, na hivyo basi akayasikiliza na kutenda kulingana na mashauri yao huku akituma barua katika majimbo yote 127 na kwa lugha zote zilizokuwepo katika Milki ile, akitilia mkazo kwamba kila mwanamume aitawale nyumba yake na kudhihirisha mamlaka yake. (12-22).

Sehemu Ya 3: Mrembo Wa Uajemi

Ili kumchagua malkia mpya, tamasha za urembo zilifanyika kote katika Milki. Hata hivyo, tamasha hizi haikuwa za kawaida: Wanawake wote warembo na wenye kuvutia katika Milki ile

wangelifanyika kuwa suria wake mfalme. Halafu yeye angalikutana nao kwa hali ya ngono ili yeye afanye uamuzi kuhusu ni nani aliyempenda zaidi na kumfanya kuwa Malkia wake. (2:2-4a). Nitafafanua zaidi juu ya upokezi wake mfalme, *'neno hilo likampendeza mfalme, naye akafanya hivyo.'(*4b)

Tamasha hii ya mashindano ya urembo ilikuwa ni kitendo katili cha kuwalazimisha wanawake katika usuria wake mfalme. Uhusiano ambao wafalme wa siku hizo za zamani waliokuwa nao pamoja na hawa wanawake wengi haukufanana na ule wake mume na mke. Mfalme wa siku hizo kama huyu Arteshasta alikuwa na makundi mawili ya kisuria, ambayo tunaweza kuyataja kama suria wa kundi la A na suria wa kundi la B. Wakati hawa wanawake walipotwaliwa katika Milki ile yote, wao waliishi katika kundi la suria A. mahali ambapo walipewa vifaa vya utakaso kwa mwaka mmoja. Hapo baadaye, wangalipelekwa kwake mfalme kwa ngono ya usiku mmoja tu. Na usiku uliofuatia wangalirudishwa katika kundi la suria B, ambapo wangaliishi maisha yao yote, wakimwona mfalme wakati yeye mwenyewe tu ndiye angalichagua yule ampendezaye. Wakati mwingi mfalme alikuwa mlevi chakari hivi kwamba hata hangelifahamu kana kwamba palikuwepo na mtu ye yote pale. Kutokana na mtazamo wa kifalme, kusudi la maisha yake yule mwanamke lilikuwa ni ule usiku mmoja tu aliokuwa pamoja naye mfalme ambao hakuukumbuka.

Watu wengine ambao tunakutana nao ni Mordekai, Myahudi mtoro, pamoja na mpwake mrembo wakuvutia kwa jina Esta, ambaye alimlea tangu kifo cha wazazi wake. Esta kwa hakika alikuwa ni mrembo wa kuvutia mno, na hivyo basi alilazimishwa katika tamasha ile ya mashindano ya mfalme ya urembo. Mordekai alikuwa amemshauri huyu Esta asije akamwambia mtu ye yote kwamba yeye alikuwa Myahudi. Siri hii itadhihirisha umuhimu wake katika ulinzi wake Mungu kwa maisha yake Esta.

Esta alipokwenda kwake mfalme Ahusuero, ni wazi kwamba mfalme alipendezwa naye hivi kwamba akamfanya yeye kuwa Malkia wa Medi-Uajemi. Hapa Mungu alikuwa amemweka mwanamke mchanga na Myahudi katika enzi mmojawapo ya nchi kuu sana ulimwenguni. (Miaka mingi baadaye, Arteshasta mwingine, mwanawe Esta, atampa ruhusa Nehemia kurudi ili kuzijenga kuta zilizouzunguka mji wa Yerusalemu.)

Siku moja, wakati Mordekai alipokuwa amekaa kwenye lango lake mfalme, aliwasikia watu wawili wakipanga kumwangamiza mfalme. Ndipo Mordekai akamwambia Malkia Esta, ambaye

alimfahamisha mfalme baadaye. Maisha yake mfalme yalinusurika, kutoka kwa wenye hila hii ya kumwangamiza mfalme ambao waliuawa. Tendo hili njema lake Mordekai lilinakiliwa katika daftari ya mambo ya nyakati yake mfalme, lakini tukio hili halikupelekwa mbele yake mfalme na kumpa dhawabu kwa tendo lake njema. Tukio hili pia litathibitisha kuwa tendo lenye kuhusika kwake Mungu kwa njia ya makusudio yake katika hadithi hii ya kuvutia.

Sehemu Ya 4: Utakaso Wa Uajemi

Hapa tunakutana na mhusika mwingine katika mchezo huu wa kuigiza, mtu katili anayefahamika kama Hamani, mmojawapo wa washauri wakuu wake mfalme. Yeye alipokuwa akitembea barabarani, alimtaka kila mmoja amsujudie. Nao watu wote walifanya hivyo –isipokuwa Mordekai, ambaye alikataa kata kuivunja ile amri yake Bwana ya kumsujudia ya Mungu peke yake (tazama Kutoka 20:3-4).

Hamani alijawa na hasira na akaapa kumwangamiza sio tu Mordekai bali na watu wake wote. (Esta 3:5-6). Alimshawishi mfalme kuitoa amri kwamba Wayahudi wote katika Milki ya Uajemi wangeliuawa siku ya kumi na tatu ya mwezi wa kumi na mbili yaani mwezi wa Adari mwaka uliofuatia (7-11). Yeye pamoja na mfalme wakaipiga kura, au kuicheza dadu, ili kuithibitisha siku. Katika lugha ya Uajemi, neno, 'kuitupa dadu' ni 'Pur.' Karamu ya 'Purimu,' ambayo inasheherekewa hata siku ya leo, hulipata jina lake kutokana na tukio hili ambalo lingemaanisha kuangamizwa kwa Wayahudi.

Wakati Mordekai alipojua mambo hayo yote yaliyofanyika, alizirarua nguo zake, akajivika gunia pamoja na majivu, na akatoka hata kufika katikati ya mji, akalia kwa sauti kuu ya uchungu. (4:1). Kote katika majimbo yale 127 ya Medi-Uajemi, Wayahudi walikuwa katika maombolezo, na kufunga, na majonzi, huku wamegandamizwa na kukata tamaa.

Esta aliposikia kwamba Mordekai alikuwa akiomboleza na kulia huku amevaa gunia, alimtuma mjumbe ili apate kufahamu yale yaliyokuwa yakiendelea. Na kwa majibu yake Mordekai alimweleza yule mjumbe kwamba Esta awatetee mbele yake mfalme kwa niaba yao Wayahudi wote waliokuwa katika Milki ya Uajemi. Esta, kwa kumjibu, kwamba ye yote yule ambaye angelitokea mbele zake mfalme bila ya ruhusa yake angaliuawa, isipokuwa yeye ambaye mfalme atamnyoshea fimbo ya dhahabuili aishi; na kwa hali ya Esta, alikuwa hajaitwa mbele yake mfalme kwa mwezi mzima (4:11). Mordekai aliwapatia wajumbe wale ujumbe wa kuvutia kumwambia Esta hivi: *'Wewe usijidhanie kwa wewe utaokoka nyumbani mwa mfalme, zaidi ya Wayahudi wote. Kwa maana wewe*

ukinyamaza kabisa wakati huu, ndipo kutakapowatokea Wayahudi msaada na wokovu kwa njia nyingine; ila wewe utaangamia pamoja na mlango wote wa baba yako; walakini ni nani ajuaye kama wewe hukuujia ufalme kwa ajili ya wakati kama huo?' (12-14).

Hivyo basi, Esta akamwuliza Mordekai kuwakusanya Wayahudi ili kuomba na kufunga pamoja naye, naye angaliomba na kufunga pia. *'Kisha nitaingia'* akamwambia, *'Nitaingia kwa mfalme, kinyume cha sheria nami nikiangamia, na niangamie.'(*16).

Wakati Esta alipokwenda mbele zake mfalme, Ahasuero kwa upendo mwingi alimnyoshea fimbo ya dhahabu na kumhakikishia kwamba angetatua hitaji lake hata kama ingalikuwa ni kumpa nusu ya Milki yake. (5:1-3). Kwa hivyo, alimwalika yeye na Hamani kwa karamu aliyowaandalia. Na hapo kwa mara nyingine mfalme akamwuliza Malkia dua yake ni lipi, lakini Esta alimwalika yeye pamoja naye Hamani kwa siku nyingine ya karamu, ambapo alimwahidi kumweleza Mfalme Ahasuero kile alichokuwa akikitaka (5:6-8).

Hamani alikuwa amepandwa na hamaki kwa kuwa alikuwa amechaguliwa na kukaribishwa katika karamu hiyo kuu na ya faragha naye Malkia na Mfalme! Lakini dharau yake Mordekai ilizidi kumweka kinyongo na uchungu mwingi. Alipowasili nyumbani kwake baada ya karamu kwa siku ile ya kwanza, alieleza kukata tamaa kwake na kutiwa uchungu naye Mordekai. Jamii yake pamoja na marafiki zake walimtia moyo ili aufanyizwe mti wa mikono hamsini urefu wake wa kumtundika huyu Mordekai, kisha awasili kazini asubuhi na mapema siku iliyofuatia na kumwuliza mfalme ampe ruhusa ili apate kumtundika juu yake. (14). Hivyo basi, Hamani akaufanyiza mti wa kumtundika usiku ule.

ONYESHO LA PILI

Uongozi Wake Mungu

Katika sura ya 6, uongozi wake Mungu unafanyika kuwa somo kuu katika kitabu cha Esta. Na kwa uongozi wake Mungu usiku huo huo baada ya karamu ya siku ya kwanza pamoja na Esta na Hamani, mfalme hakuupata usingizi. Ndipo akaamuru aletewe kitabu cha maandiko ya taarifa nayo yasomwe mbele yake. Ikaonekana kuwa imeandikwa kuwa Mordekai aliwachongea wasimamizi wawili wa mfalme waliotaka kumtia mikono mfalme Ahasuero. Wakati mfalme aalipogundua kuwa ni

Mordekai aliyezuia mauaji yake, aliuliza ni heshima gani au jaha gani aliyofanyiwa kwa ajili ya hayo? Pia aliuliza ni nani aliyekuwa ndnai ya behewa wakati huo. Mtumishi wake akasema kwamba Hamani alikuwa tayari amewasili kazini mapema.

Sehemu Ya 1: Mageuzi Ya Meza

Huku akitaka kumheshimu Mordekai, Ahasuero alimwalika Hamani (ambaye alikuwa katika jumba lile kumwomba ruhusa mfalme ili apate kumtundika Mordekai) na akaulizwa hivi, *'afanyiziwe nini yule ambaye mfalme apenda kumheshimu?'* Hamani, alifikiria kwamba yeye ndiye aliyekuwa mtu ambaye mfalme alitaka kumheshimu. Hivyo basi, akampatia wazo hili kuu. *'Na aletewe mavazi ya kifalme ambayo mfalme amezoea kuyavaa,na farasi ambaye mfalme humpanda mwenyewe,ambaye ametiwa taji ya kifalme kichwani na yale mavazi na yule farasi akabidhiwe mkononi mmojawapo wa maakida wa mfalme aliye mstahiki; ili makusudi amvike yule ambaye mfalme apenda kumheshimu, na kumkaribisha juu ya farasi kuipitia njia kuu ya mjini, na kupiga mbiu mbele yake, kusema, Hivyo ndivyo atakavvvyofanyiziwa mtu yule ambaye mfalme apenda kumheshimu.* (6-9).**'** *'Hima! Twaa mavazi na farasi kama ulivyosema, ukamfanyizie vivyo hivyo Mordekai.'* Mfalme akamwambia hivyo huyu Hamani aliyeshushwa kiasi hicho na kuduwaa. (10) Ndipo alitii na baadaye akaharakisha kurudi nyumbani mwake, kwa wakati huu akiwa na woga. Na baada ya kufika nyumbani alipata mwaliko mwingine wa pili kutoka kwa Esta kwa karamu nyingine.

Katika karamu hiyo, mfalme kwa mara nyingine akamwuliza Esta dua yake ilikuwa nini. Esta akajibu kwamba alitaka maisha yake pamoja na ya watu wake kuwa dua na haja yake. 7:3-4). Ndipo mfalme aliponena akasema*, 'Ni nani huyu, tena yuko wapi, ambaye moyoni mwake alithubutu kufanya hivi? Esta akasema, Ni mtesi, tena ni adui, ndiye huyu Hamani, mtu mbaya kabisa.'*

Hamani kwa hakika alifahamu kwamba yeye amefikia ukingoni. Na kwa hasira kuu, Ahasuero akaondoka katika ghadhabu yake kutoka kwenye karamu. Huku akijitakia maisha yake kwa malkia Esta, kwa kuwa aliona ya kwamba amekusudiwa madhara yake mfalme. Ikiwa amejitupa chini penye kitanda alipokuwapo Esta. Wakati mfalme aliporudi alimpata Hamani penye chini ya kitanda chake Esta na kusema, *Namna gani! Je! Utamfanyia malkia jeuri hata machoni pangu nyumbani mwangu?* (8) Mmoja wa wasimamizi-wa-nyumba ya mfalme akasema kuhusu mti alioufanyiza kwa ajili ya kumtundika Mordekai juu yake. Mfalme akaitoa amri kwamba Hamani apate kutundikwa juu ya mti ule! (9-10)

Sehemu Ya 2: Amri Ya Wokovu

Wayahudi waliokuwa wakiishi Uajemi bado walikuwa na shida–Ile amri ya kuangamizwa kwao. Kwa kuwa ile sheria ya Wamedi na Waajemi haingebatilishwa, Ahasuero, Esta na Mordekai waliandika sheria nyingine ya pili iliyowaruhusu Wayahudi kujilinda wenyewe na kuwaangamiza maadui wao siku hiyo ya kumi na tatu ya mwezi ya mwezi wa kumi na mbili yaani mwezi wa Adari. (Sura 8). Sasa ilikuwa ni Julai, na kwa muda wa miezi sita, wajumbe wake mfalme wangelikuwa wamewasili katika kila pembe ya Milki ile wakiwa na habari njema: hapa upo ujumbe wa uhai kwake kila Myahudi ambaye yupo chini ya amri ya mauti. Amri hii ya uzima iliyaokoa maisha yao Wayahudi wote. (Mwanzo 12:3).

Matumizi Ya Kibinafsi

Ni mambo yapi ya kutazama katika kitabu hiki chenye kuvutia sana cha Esta? Kwanza, tunahitajika kueneza habari kuhusu tangazo lake Yesu la uhai kwa ulimwengu ulio na watu walio chini ya amri ya mauti.

La pili, tunaweza kuwa na pumziko katika matimizo ya ahadi zake Mungu. Esta ni mfano bora wa picha ya matimizo ya ahadi yake Mungu katika agano lake kwake Ibrahimu ili kuwabariki wale wenye kumbariki yeye na kuwalaani wale wenye kumlaani yeye (Mwanzo 12:3).

La tatu ni ile kanuni kuu kwamba inawezekana kutendeka kinyume. Kifo chake Hamani ni mfano mouvu kuhusu kanuni kuu: (Watendee wengine jinsi ungependa wao wakutendee wewe): ‘Usilitende jambo lo lote ambalo haungelimpenda ye yote akutendee wewe.’

Jambo la nne, ni ulinzi wake Mungu juu ya wale wenye kumpenda na kumtii yeye. Mtume Paulo alisema haya: *‘Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.’* (Warumi 8:28) Hata wakati ambapo Esta alipolazimishwa kujiunga na tamasha ile katili ya urembo, Mungu bado alikuwa ndiye mwenye usukani katika maisha yake, huku akitimiza kusudi lake njema – ambayo ilifanyika na kuwa ukombozi wa nne kwa Wayahudi kutokana na janga la maafa.

Uongozi wake Mungu katika mazingira ya maisha yako na yangu ni mojawapo ya ujumbe muhimu katika kitabu cha Esta. Je, unaamini kwamba Mungu huyatenda yale apendayo katika hali zote za maisha yako? Lipo sharti ili kuipokea hii ahadi. Ikiwa wewe humpendi Mungu na kuyafuata makusudio na mipango yake, yeye hatayafanya mambo yote kufanyika kwa wema. Lakini ikiwa utampenda Yeye, na kudhihirisha upendo wako kwake kwa kuitwa kulingana na mapenzi yake na njia zake, hivyo basi, unaweza kuamini kwamba yeye atakiweka cho chote katika maisha yako kwa mipango yake iliyo njema–njema kwake na hatimaye iliyo njema kwako pia.